# MATUMIZI YA LUGHA YA ISHARA KATIKA NYIMBO ZA TAARABU: UCHUNGUZI WA NYIMBO ZA MOHAMED AHMED MOH'D

**ASHA RAMADHAN ALI**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA IDARA YA KISWAHILI KWA AJILI YA KUKIDHI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA TANZANIA**

**2018**

## ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasnifu hii iitwayo kuchunguza **Matumizi ya Lugha ya Ishara Katika Nyimbo za Taarabu: Uchunguzi wa Nyimbo za Mohamed Ahmed Moh'd** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya kupatiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Isimu ya Kiswahili ya Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

**…………………………………………….**

**Dkt. Mohamed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

**Tarehe…………………………………**

## TAMKO

Mimi **ASHA RAMADHAN ALI** nakiri kwamba tasnifu hii ni yangu niliyoifanya kwa juuhudi zangu mwenyewe haijawahi kuwasilishwa na mtu mwengine kwa mahitaji ya shahada ya aina yoyote kutoka katika chuo chochote kile.

**SAINI …………………………………………………………**

**TAREHE……………………………………………………**

## TABARUKU

Tasnifu hii nawatunuku wazazi wangu mama yangu Hanuni Abdulla Haji na Marehemu baba yangu Ramadhan Ali Abdulla kwa malezi bora waliyonilea na kunipa elimu bora. ALLAH awalipe yenye kheri tupu. Aidha naitabarukia familia yangu mume wangu Ahmed Shaha Ahmed na watoto wangu Abdul-latif, Rahila, Rihaam kwa kunipa furaha na kunitoa uchovu katika kipindi chote cha masomo yangu Mwenyezi Mungu awakuze na awazidishie ufahamu wa elimu ya duniani na Akhera.

**SHUKURANI**

Kwa heshima na unyenyekevu sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mola mtukufu ambae hakuna mfano wake kwa kunijaalia nguvu na uwezo wa kuifanya kazi hii kwa afya njema kabisa. Matunda ya kazi hii ya utafiti wa matumizi ya lugha ya ishara aliyoitumia mtunzi Mohammed Ahmed Mohammed katika nyimbo za taarab asilia yametokana na mashirikiano makubwa kati ya waimbaji, wapenzi na mashabiki wa vikundi mbali mbali vya taarab asilia bila ya kuwasahau wanafamilia wa mtunzi huyu mashuhuri wa nyimbo za taarab asilia.

Hata hivyo kazi hii isingeweza kukamilika bila ya msaada wake yeye mwenyewe pamoja na wasanii, wapenzi na watu wa karibu wa mtunzi huyu Mohammed Ahmed ambao walikubali kufanya kazi bila ya kuchoka.Kwa hivyo napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wale wote walionisaidia, ingawa ni watu wengi na sirahisi kuwaleza wote lakini kwa niaba yao nitawataja baadhi ili wawe ni kiwakilishi kwa wenzao.

Shukurani zangu za awali nazitoa kwa walimu wa chuo kikuu Huria cha Tnzania (Open University of Zanzibar, kwa kunipa taaluma hii na kwa juhudi zao walizozichukua kwa kuja Unguja na kutusomesha kwa kiwango kinachostahiki. Bila ya kumsahau Dr Anna Kishe ambaye alitupatia maarifa haya ya utafiti kinadharia. Shukurani za pekee kwa msimamizi na muongozaji wa kazi hii ambae ni Dkt. Mohammed Omar kwa miongozo yake na ustahamilivu na uvumilivu wake katika kuipokea kazi. Halikadhalika napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Prof. M. T. Y. Sengo kwa ushauri na maelekezo yake katika uteuzi wa mada na kutuongoza na kutusimamia ipasavyo wakati wa kipindi chote cha masomo.

Shukurani zangu za pili nazitoa kwa wanafunzi wenzangu wote tuliokuwa pamoja katika kipindi chote cha masomo ya ngazi hii ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu huria, wa upande wa sarufi na fasihi ambao walionyesha mashirikiano ya pamoja katika kuhakikisha kuwa tunamaliza pamoja salama usalimini, juhudi zao zimeonyesha ari ya kutaka kutafiti zaidi katika lugha hii ya Kiswahili. Bila ya kuisahau Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa kutupa ruhusa maalumu ya kuingia darasani katika kipindi chote ambacho walimu wetu walikuja kwa kutusomesha tunawashukuru sana.

Shukurani za tatu nazitoa kwa familia yangu, ndugu, jamaa zangu na hasa mama yangu mpendwa kwa kunihamasisha na kuniunga mkono katika suala zima la kupata elimu ya juu kwa hakika huyu ni mama mwema. Bila ya kumsahau mume wangu mpenzi ambae aliniruhusu bila ya kinyongo na kuniwezesha kwa kuhudhuria darasani katika kipindi chote cha masomo na kunipa msaada wake mkubwa ulionifanya niione nyepesi hasa kwa vile alijitahidi kuzikusanya nyimbo nyingi za mtunzi huyu na kunielekeza vya kufanya. Mwenyezi Mungu amzidishie mapenzi na Imani, Amin. Nitakuwa mwizi wa fadhila endapo sitowashukuru wanafamilia wa mtunzi huyu Mohammed Ahmed Mohammed ambae sasa ni marehemu kwa msaada wao na mashirikiano yao makubwa katika kipindi chote kazi hii ilipokuwa inatafitiwa mpaka kumalizika kwake ambapo msanii huyu alifariki wakati ikimaliziwa ripoti yake. Mbali ya hayo Marehemu Mohammed Ahmed wakati wa uhai wake alinipa mashirikiano ya hali ya juu ikiwa ni pamoja na kunipatia historia yake na kunipa nyimbo mbalimbali za taarab asilia alizozitunga akiwa katika kikundi cha CULTURE MUSICAL CLUB na nyengine akiwa NARD IKHWAN SWAFAA

(malindi) ambazo kati ya hizo kuna zile alizozitunga yeye mwenyewe na kuna zile alizowatungia waimbaji wengine wakaziimba nao wakapata umaarufu wa kujulikana kupitia nyimbo hizo.

Mwisho kabisa napenda kuwashukuru walimu wenzangu wa skuli ya Kiembe Samaki Sekondari kwa msaada wao mkubwa bila kumsahau malimu mstaafu ALI KHAMIS SHAALI ambae aliichukuwa bidii ya kunitafutia kazi tangulizi na kuniongoza katika uandishi wa ripoti ya utafiti huu, mbali na hayo sitowasahau wakutubi wa Baraza la Kiswahili Zanzibar kwa kuniruhusu kwa muda wote wa utafiti huu kuitumia maktaba yao kila nilipoihitaji.

Katika ukurasa huu mdogo ni vigumu kuwataja wale wote walionisaidia kwa namna moja au nyengine katika kufanikisha utafiti huu, hata hivyo nawaomba wote wazipokee shukurani hizi.

## IKISIRI

Mtunzi wa kazi ya fasihi ni mtu muhimu sana na kazi yake ya fasihi huwa ni jicho la jamii. Hivyo anaitumia sanaa yake ya utunzi kiubunifu zaidi katika kuyaeleza yale yanayoikumba jamii yake. Moja kati ya mbinu anazozitumia mtunzi wa kazi ya fasihi ni matumizi mazuri ya lugha ya ishara. Utafiti huu umelenga katika kuzibainisha ishara zilizotumika katika nyimbo za taarab asilia zilizotungwa na mtunzi Mohammed Ahmed Mohammed. Tasnifu hii imebainisha wazi jinsi ishara hizo zilivyojengwa kupitia nadharia ya Semiotiki, katika kuzieleza ishara hizo zilizomo katika utunzi wake, mtafiti ametumia nyimbo kadhaa zilizotungwa na msanii huyu alizozipata kupitia watafitiwa wake na nyengine alizozipata kutoka kwa mtunzi mwenyewe na kuzibainisha ishara hizo na dhima zake kwa maisha ya jamii ya sasa.

Lengo kuu la utafiti huu ni kubainisha matumizi ya lugha ya ishara yaliyotumika katika nyimbo zilizotungwa na Mohammed Ahmed na kuzibainisha ishara hizo kwa kuzifafanua ili kujuwa makusudio ya nyimbo yenyewe na kuzielezea kiashiria cha ishara hizo na dhima zake kwa jamii ya sasa. Mada hii iliyoteuliwa kwa misingi kwamba kazi ya fasihi huibua maana ya kisemiotiki na kuwa nyimbo zilizopendekezwa hazijawahi kufanyiwa uhakiki wa ishara kwa mtazamo wa nadharia ya kisemeotiki, mfano wa nyimbo zilizofafanuliwa ni, kibiriti na petrol, Nanasi, Nampenda kumwambia siwezi, Kunguru, Kanikimbia, Nilikuchagua, Kisebusebu, Sikujuwa kama mapenzi matamu, Lishalo haliji tena, Kweli alikuwa wangu, Mpenzi wangu hawezi, Komamanga, Ndege wangu, Ndege karuka karudi. Tasnifu hii imejengwa na sura tano ambapo katika sura ya kwanza imepangiliwa na usuli wa mada, Kauli ya utafiti, Malengo ya utafiti, Umuhimu wa utafiti, Maswali ya utafiti na mipaka ya utafiti. Katika sura ya pili imepangwa kwa Mapitio ya kazi tangulizi, Fasihi na lugha, nadharia ya utafiti. Kwa upande wa sura ya tatu imejengwa kwa Mbinu za ukusanyaji wa data, usanifu wa utafiti eneo la utafiti, aina ya data zilizokusanywa, mbinu za kukusanyia data za upili, uchambuzi wa data, sampuli na usampulishaji. Sura ya nne inahusisha uchambuzi wa data za awali na za upili, ambao umejumuisha nyimbo zilizokusanywa na zilizofafanuliwa na watafitiwa. Sura ya mwisho imekamilisha kazi hii kwa kutoa matokeo ya utafiti huu ambayo yametoa aina ya ishara zilizopatikana katika nyimbo za msanii huyu pamoja na kutoa matatizo na mapendekezo ya utafiti.

## YALIYOMO

ITHIBATI ........................................................ i

TAMKO ........................................................ ii

TABARUKU ........................................................ iii

SHUKURANI ........................................................ iv

IKISIRI……. ........................................................ vii

YALIYOMO ........................................................ viii

ORODHA YA MICHORO ........................................................ xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........................................................ 1**

1.1 Utangulizi wa Jumla ........................................................ 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........................................................ 4

1.3 Kauli ya Tamko la Utafiti ........................................................ 9

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................ 10

1.4.1 Lengo Kuu ........................................................ 10

1.4.2 Malengo Mahususi ........................................................ 10

1.5 Maswali ya Utafiti ........................................................ 10

1.6 Umuhimu wa Utafiti ........................................................ 10

1.7 Mipaka ya Utafiti ........................................................ 11

1.8 Mpangilio wa Tasinifu ........................................................ 11

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ........................................................ 13**

2.1 Utangulizi ........................................................ 13

2.2 Ufafanuzi wa Dhana Mbalimbali ........ 13

2.2.1 Fasihi na Lugha ........ 13

2.2.2 Nyimbo na Harusi ........ 15

2.3 Taswira na Lugha ya Ishara katika Fasihi ........ 24

2.4 Mkabala wa Kinadharia ........ 27

2.4.1 Mihimili ya Nadharia ya Semiotiki ........ 29

2.5 Hitimisho ........ 39

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 41**

3.1 Utangulizi ........ 41

3.2 Usanifu wa Utafiti ........ 41

3.3 Eneo la Utafiti ........ 42

3.4 Kundi Lengwa ........ 43

3.4.1 Sampuli na Usampulishaji ........ 43

3.5 Aina ya Data Zilizokusanywa ........ 44

3.5.1 Data za Msingi ........ 44

3.5.2 Mbinu za Kukusanyia Data za Msingi ........ 44

3.5.3 Data za Upili ........ 45

3.6 Uchambuzi wa Data ........ 45

3.7 Hitimisho ........ 46

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA WA DATA ZA UTAFITI ........ 47**

4.1 Utangulizi ........ 47

4.2 Uainishaji wa Nyimbo na Ufafanuzi wa Lugha ya Ishara ............................. 47

4.2.1 Wimbo wa Kwanza: KIBIRITI NA PETROLI............................................. 47

4.2.2 Wimbo wa Pili: NANASI ................................................................... 49

4.2.3 Wimbo wa Tatu: NAMPENDA KUMWAMBIA SIWEZI........................... 52

4.2.4 Wimbo wa 4: KUNGURU.................................................................... 54

4.2.5 Wimbo wa 5: KANIKIMBIA ............................................................... 55

4.2.6 Wimbo wa 6: NILIKUCHAGUA .......................................................... 57

4.2.7 Wimbo wa 7: KISEBUSEBU ............................................................... 59

4.2.8 Wimbo wa 8: SIKUJUA KAMA MAPENZI MATAMU ............................. 60

4.2.9 Wimbo wa 9: LISHALO HALIJI TENA.................................................. 61

4.2.10 Wimbo wa 10: NDEGE KARUKA KARUDI.......................................... 63

4.2.11 Wimbo wa 11: KOMAMANGA ........................................................... 65

4.2.12 Wimbo wa 12: NDEGE WANGU ........................................................ 67

4.2.13 Wimbo wa 13: KUKUPENDA SANA .................................................. 69

4.2.14 Wimbo wa 14: KWELI ALIKUWA WANGU.......................................... 70

4.2.15 Wimbo wa 15: MPENZI WANGU HAWEZI .......................................... 72

4.2.16 Wimbo wa 16: KUDAGANYWA NIMECHOKA....................................... 75

4.3 Hitimisho.............................................................................................. 77

**SURA YA TANO: HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO .......... 78**

5.1 Utangulizi............................................................................................ 78

5.2 Matokeo ya Utafiti ................................................................................ 78

5.2.1 Aina za Ishara....................................................................................... 78

5.2.1.1 Ishara ya Mahusiono ........................................................................... 78

5.2.1.2 Ishara ya Ujasiri katika Mapenzi ........ 79

5.2.1.3 Ishara ya Mapenzi ya Udanganyifu ........ 79

5.2.1.4 Ishara ya Kukataliwa katika Mapenzi ........ 80

5.2.1.5 Ishara ya Hisia za Mapenzi ........ 80

5.3 Hitimisho ........ 80

5.4 Mapendekezo ........ 80

**MAREJELEO ........ 82**

**VIAMBATISHO ........ 86**

## ORODHA YA MICHORO

Mchoro A: Ishara, kiashiriwa na kiashirii ........................................................ 30

Mchoro B: Piramidi ya Peirce ya kufasiri ishara ................................................ 32

Mchoro C: Mihusianisho ya kufasiri ishara. ...................................................... 34

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi wa Jumla

Lugha ni nyenzo kuu katika fasihi na kwa mhakiki basi ni muhimu kuitambua nafasi hii kubwa. Msingi hasa wa fasihi ni uhuru wa mwandishi wa kuweza kuchota kutoka kwenye hazina pana. Kwa mujibu wa wanaurasimu wa kirusi ambao wana kuwa lugha ya kifasihi inatofautiana na lugha ya kawaida kwa kuwa zipo mbinu za kuiajinabisha lugha hii. Sifa hii inahusishwa zaidi na ushairi ambao kutokana na kawaida na kanuni za kimuundo lugha inayotumiwa inaweza kuonekana tofauti na lugha ya kila siku (Wamitila, 2008, uk.68).

Uhusiano kati ya lugha na fasihi ni wa lazima kazi na sanaa inayotumia maneno, kwa kiwango kikubwa zimeathiri makuzi na maendeleo ya lugha. Imethibitishwa kwa mifano bayana na isiyo mushkeli kwamba utamaduni wa waswahili ikiwemo lugha yao ulizaa mfano bora wa mwanaadamu, alikua mtunzi au bwana wa sanaa za aina nyengine, mshairi wa kupigiwa mfano, mwimbaji mwenye kipaji. Wakati huo huo jamii yake ilimdai kuonyesho uwezo usio doa wala toa katika kuitawala lugha ya Kiswahili.Awe na hazina ya methali, vitendawili na mashairi na pia amiliki uwezo wa kuunda au kutumia maneno yaliyobuniwa (Haji 1989).

Tukitaka kumuelewa vyema mwandishi, hatuna budi kuyaelewa maisha yake. Haijawahi kutokea kwamba mtunzi au msanii kujaaliwa na kipawa tu bila ya kipawa kuathiriwa na mambo kadhaa yaliyomzunguka kama vile ukoo wake, majirani, chuoni alikokwenda kusoma qur-ani, marafiki aliozoeana nao, michezo aliyocheza na mambo mengineyo.

Mohammed Ahmed Mohammed amezaliwa tarehe 12-05-1940 katika mtaa wa Kiembe samaki katika mkoa wa Mjini magharibi B Unguja, amepata elimu yake ya msingi katika skuli ya Kiembe samaki mnamo mwaka 1947 na elimu ya Junior katika skuli ya Sekondari ya Benbella.Pia mnamo mwaka 1962 alijiunga na chuo cha ualimu cha Nkurumah kwa mafunzo ya ualimu na aliajiriwa kama mwalimu katika skuli mbali mbali za Zanzibar, miongoni mwa skuli alizosomesha ni Kiembe samaki, Langoni... Mnamo mwaka 1976-1979 alijiunga na masomo ya shahada ya kwanza katika chuo kikuu cha Dar es salaam na aliwahi kupata mafunzo ya shahada ya pili katika chuo cha Institute of social studies huko Nether land mnamo mwaka 1979-1984 alianza kutunga mashairi akiwa na umri wa miaka 19 wakati mwanafunzi wa kidato cha tatu. Mtunzi huyu mkongwe aliwahi kupata tunzo mbali mbali, tunzo yake ya awali aliipata kabla ya mapinduzi, aliposhiriki kutunga mashairi yaliyochapishwa katika gazeti la maarifa na ushairi wake aliupa jina la NYOTA NA FAKHARI. Mnamo mwaka 1963 alikua tayari mzoefu katika fani hii ya utunzi. Kwa mujibu wa maelezo yake kazi hii ya utunzi hakuna aliyemfundisha na alitunga mashairi ya harusi zaidi, mashairi yake ni ya kimapokeo na kimamboleo katika mtindo wa tathlitha, tarbia na takhmisa.

Miongoni mwa kazi alizowahi kufany ni ualimu kuanzia mwaka 1976-1979 kwa vile alikua ni msanii msomi aliwahi kufanya kazi katika wizara ya utamaduni kama Afisa wa mambo ya kale mwaka 1982. Katika mwaka huo huo alichaguliwa kuwa katibu wa Raisi wakati wa uwongozi wa Mh.Aboud Jumbe Mwinyi, mnamo mwaka 1984 alikua katibu wa Rais Mh. Ali Hassan Mwinyi, mnamo mwaka 1985 alikua katibu mkuu ofisi ya makamo wa pili wa Rais mwaka 1990 alikua katibu wa Rais wakati

wa Mh.Dkt Salmin Amour Juma. Kazi ambayo aliifanya mpaka kustaafu kwake wakati alipomaliza uwongozi Dkt.Salmin Amour Juma alistaafu mwaka 1996, kutokana na utumishi wake kuwa bora aliteuliwa kufanya kazi katika tume ya utumishi serikalini. Alikua ni mjumbe wa baraza la Kiswahili Zanzibar shughuli ambayo aliendelea nayo mpaka alipofariki tarehe 15-07-2017.Mwenyeezi Mungu amlaze mahali pema peponi Aamin.

Katika ulingo wa sanaa wimbo uliompatia mwanga ni Kisebusebu, aliwahi kuwa katibu mkuu wa Culture Musical Club. Alikuwa muasisi wa mwanzo wa kupigwa taarabu katika vikundi vya Culture musical club na Nard Ikhwan Safaa ili kudumisha udugu. Utunzi wa Mohammed Ahmed ni utunzi ulioendana na mwenendo na muonekano wake, kwani alikuwa ni mtu mwenye hekima na busara, mpole na mtaratibu na msomi aliyekubalika katika jamii, mvumilivu na mwenye kupenda kubembeleza. Mbali na hayo alikua maridhia kwa watu. Hali hii imepelekea hata kuathiri kazi yake ya utunzi ambayo inazionyesha tungo zake nyingi ni zenye kubembeleza, kuridhia, kusifu na kufafanua uzuri wa mapenzi. Mtunzi huyu ni gwiji katika tungo za mahaba na mapenzi ana uwezo wa hali ya juu katika kuisarifu lugha ya Kiswahili katika kutunga tungo za mahaba zenye kusisimua kutokana na uwezo wake wa kuisarifu picha inayojenga uhalisia kwa msomaji.

Kutokana na kipaji chake aliweza kuwainua, kuwahamasisha na kuwatangaza waimbaji wengi ambao aliwatungia nyimbo na wao wakaziimba kwa mfano RUKIA RAMADHANI katika wimbo wa Nnazama,Tunapendana, Kukupenda sana, MTUMWA MBAROUK Sikujuwa kama mapenzi matamu, FAUZIA ABDALLAH aliimba lishalo haliji tena, SEIF SALIM aliimba Ndege wangu, Watu wananiuliza,

KHAMIS SHEHE aliimba Kweli alikuwa wangu, SAIDA ABDALLAH aliimba Pendo kitu cha khiari, SEIF MAALIM Pendo la kina, MAULID MOHAMMED Ilikua siku njema, Pesa imekughilibu, Ishara zanisumbua.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Adam (2009) katika tasnifu yake ya nyimbo za kizazi kipya kwa lugha ya Kiswahili amemnukuu Kipury (2000) anasema kwamba kwa hali yoyote iwayo, nyimbo haziwezi kuepuka kuelezea falsafa ya maisha ya watu wa jamii husika, imani, silka na desturi zao.

Khamis (2013) katika tasnifu yake amemnukuu Metteru (1987) ambae anaeleza kuwa nyimbo ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodi, mkongosho mapigo na muwala. Nyimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja pekee au wazumi wake wakiitikia mkarara na zinamfuatano au mpangilio maalum wa sauti, mwendo, picha na ishara. Katika kazi yake ameeleza maana na historia ya asili ya Taarabu Zanzibar, ingawa hakuzungumzia utunzi wa nyimbo za Mohamed Ahmed lakini kazi yake itatusaidia sana katika utafiti wetu kwa kujua asili ya Taarabu na utamaduni waZanzibar.

Mercer (1977) katika kitabu chake cha Beauty of Zanzibar anaeleza kwamba Zanzibar ni mkusanyiko wa visiwa vilivyoko upande wa mashariki katika bahari ya hindi. Katika kitabu chake ameeleza mipaka ya unguja na miji mikuu ya unguja na visiwa vilivyomo na wakaazi wake kwa ujumla. Katika kazi yake amezungumzia historia ya visiwa vya Zanzibar na asili ya wakaazi wake. Ingawa hakuzungumzia

utunzi wa nyimbo za taarabu lakini kazi yake itatusaidia kujua asili na shughuli za wazanzibari na mahusiano yao na jamii nyengine.

Thabit (2007) akimnukuu Khatib (1981; 16) ambae ameeleza kwamba nyimbo lazima zifungamane na mashairi simulizi. Pia nyimbo huwa na kawaida ya kueleza hisi nzito zilizomo ndani ya jamii fulani. Nyimbo zikiwemo zile za Taarab lazima zifungamane na falsafa ya jamii husika kulingana na wakati na mahitaji ya jamii hiyo. Maudhui yake yaoane na maisha ya jamii hasa utamaduni wa jamii husika. Ingawa hawakuzungumzia juu ya nyimbo zaTaarabu za Mohamed Ahmed kazi hii itatusaidia katika kupata ufafanuzi wa nyimbo na kuzipata baadhi ya nyimbo za Taarab alizozitumia Thabit ambazo zinatokana na Taarabu asilia.

Robert (1992;8-10)anaeleza kuwa Siti bint Saad ni mwanamke wa kwanza aliyepeleka Taarabu uswahilini yaani tabaka la chini katika miaka ya (1911-1919)mwanamke huyu alijiunga na jamii ya waarabu maarufu sana kwa wakati ule, kama vile Subeti Ambari aliyekuwa mpiga udi, Buda Swedi mpiga gambusi, Mwalimu Shaabani mpiga tari na Mbaruk. Ijapokuwa katika kazi yake hiyo hakumzungumzia Mohamed Ahmed na utunzi wake lakini kazi hii itatusaidia kuwajua watunzi na waimbaji wengine na nyimbo zao najinsi walivyokuwa wakiimba akiwemo mtunzi huyu Mohamed Ahmed Moh’d.

Nae Khamis (2013) amemnukuu Jilala(2008;114)katika tasnifu yake ya The artist uses of metaphors in constructing meaning and message in new generation song in Tanzania, amechambua sitiari katika nyimbo mbali mbali za muziki wa kizazi kipya alizoziteua. Katika utafiti wake amebaini kuwa nyimbo za muziki wa kizazi kipya

zinatumia zaidi sitiari ili kufikisha ujumbe haraka kwa jamii. Kazi hii itatusaidia sana katika utafiti wetu kwani kupitia kipengele hiki cha sitiari, kitatupa muelekeo wa kuchambua kipengele cha lugha ya ishara katika nyimbo za Taarabu za Mohamed Ahmed Mohamed hivyo kupitia kipengele cha sitiari tutafafanua kipengele cha lugha ya ishara zilizotumika katika nyimbo hizo.

Wamitila (2004)anaeleza kuwa ushairi huhusishwa na utendaji kwa sababu unawasilishwa kwa hadhira kwa kutegemea sauti, kuimbwa au kughaniwa.Siajabu basi tungo hizo zikaambatanishwa na ala za muziki, mapigo ya ngoma, kupiga makofi na sifa nyengine zinazohusiana na utendaji kama kubadilishwa kwa sauti na ishara ya uso.Ijapokuwa hakugusia lugha ya ishara katika nyimbo za Taarabu za Mohamed Ahmed lakini kazi hii itatusaidia katika ufafanuzi wa utumikaji wa lugha ya ishara na dhima yake katika nyimbo tutakazo zitumia ambazo ni za mtunzi huyu.

Wamitila (2008) anafafanua kuhusu lugha kuwa ni nyenzo kuu katika fasihi na kwa mhakiki ni muhimu kuitambua nafasi hii kubwa katika ukurasa huu amezungumzia jinsi lugha inavyompa uhuru mwandishi wa kazi ya fasihi kwa kutumia vionjo mbali mbali vya lugha.Ingawa hakuzungumzia utunzi wa Msanii Mohammed Ahmed kazi yake imetupa njia ya kuweza kuifafanua lugha ya ishara aliyoitumia katika utunzi wake.

Haji (1989) katika makala yake aliyomzungumzia msanii M. S. Abdulla mchango wake katika maendeleo ya Kiswahili katika kazi yake amefafanua lugha aliyoitumia katika kazi zake na kwa kiasi gani imekuza Kiswahili.Hata hivyo kutumika kwa ufafanuzi wa matumizi ya lugha aliyotumia mtunzi huyu kumeifungua kazi hii kwa

kiasi kikubwa katika kutoa ufafanuzi wa lugha ya ishara aliyoitumia mtunzi Mohammed Ahmed Mohammed katika nyimbo zake.

Khamis (2013) katika tasnifu yake inayohusu Matumizi ya mafumbo na taswira katika nyimbo za mapenzi za Taarabu asilia za Zanzibar ameeleza hitoriya ya Taarabu na historia ya kikundi cha Taarabu cha CULTURE MUSICAL CLUB katika tasnifu yake ametumia baadhi ya nyimbo zilizotungwa na mtunzi huyu bwana Mohamed, na amefafanua jinsi zilivyotumia Matumizi ya mafumbo, vile vile ametumia maelezo yanayohusu Taarabu aliyoyapata kupitia mahojiano yake yeye na bwana Mohamed Ahmed. Ingawa hakufafanua lugha ya ishara iliyotumika katika nyimbo zake lakini itatuongoza katika kupata ufafanuzi wa Matumizi ya lugha ya ishara alizozitumia mtunzi huyu katika nyimbo zake

Hassan (2007) katika utafiti wake amechunguza athari za nyimbo za msanja katika maisha ya mke na mume katika kijiji cha Jambiani.Hivyo amegundua kwamba msanja hivi sasa hausikikani katika ndoa nyingi, lakini inaonekana kuwa wanajamii hao wa kusini Unguja bado wanakubaliana kwamba, nyimbo za msanja ni msingi wa ndoa. Ingawa katika tasnifu yake hakuzungumzia lugha ya ishara katika nyimbo za Taarab za Mohamed Ahmed lakini kazi hii itatusaidia katika uchambuzi na ufafanuzi wa nyimbo tutakazozitumia.

Mvungi (2007) katika tasnifu yake nafasi ya nyimbo za singarimbwa katika jamii ya watumbatu, sehemu ya Gombani ambapo mafunzo yake yanauhusiano mkubwa najamiimya watumbatu. Ijapokuwa katika kazi yake hakuzungumzia nyimbo za

Taarabu lakini itatusaidia katika ufafanuzi wa nyimbo kwa vile Mdungi amezifafanua nyimbo zake.

Juma (2008) katika tasnifu yake amezungumzia nafasi ya nyimbo za unyago katika jamii ya Wazanzibari katika zama za utandawazi.Katika tasnifu yake amezizungumzia kuhusu nyimbo za unyago ambazo huimbwa ili kuonesha furaha ya kutoka tabaka moja la jamii hadi jengine.Ingawa hakuzungumzia lugha ya ishara iliyotumika katika nyimbo za Taarabu lakini tasnifu yake itatusaidia katika kuzifahamu nyimbo na ufafanuzi wake unavyohusiana na uhalisia wa maisha.

Saleh (2015) katika kitabu chake cha maisha ya msanii Haji Gora ambapo amezungumzia tangu uzawa wa mtunzi huyu ,maisha yake na utunzi wake kwa ujumla.kazi yake imetuongoza katika kundika historiya ya mtunzi huyu kwa umakini kwa vile na yeye ni mtunzi wa nyimbo ambazo zimeimbwa katika vikundi mbali mbali vya taarab.

Khatib (1992) amezungumzia juu ya historia ya Taarabu Zanzibar ambapo pamoja na hayo ameeleza vikundi vya awali vya Taarabu na historia za uanzishwaji wa vikundi hivyo,vile vile katika kitabu chake ametoa baadhi ya nyimbo za Taarabu zilizotungwa na watunzi wa Taarabu wa Zanzibar akiwemo Bwana Mohamed Ahmed.Mbali ya kutozungumzia lugha ya ishara iliyotumika katika nyimbo hizo ,kazi hii itatusaidia katika kupata historia ya Taarab Zanzibar pamoja na vikundi vyake.Halikadhalika baadhi ya nyimbo alizozitumia Khatib ni miongoni mwa nyimbo zilizotungwa na Mohamed Ahmed Moh’d ambazo zitatusaidia katika ufafanuzi wa kazi hii.

Katika tovuti ya h.t.t.p/w.w.w.gafkosoft.com>imeeleza maana ya nyimbo na ufafanuzi wa uimbaji na utunzi wa nyimbo ambao unaambatana na sifa za nyimbo.Hivyo ingawa kazi hii haikuzungumzia lugha ya ishara inayotumika katika nyimbo za Taarab za Mohamed Ahmed lakini itatusaidia katika ufafanuzi wa nyimbo kupitia sifa za nyimbo na kupelekea kupata urahisi wa ufafanuzi wa matumizi ya lugha ya ishara hiyo kwa jamii.

Khatibu (2014) katika kitabu chake ameeleza asili ya Taarabu Zanzibar, Taarabu katika vipindi mbalimbali vya maisha ambapo amefafanua juu ya kukua na kuenea kwake.Ingawa hakujikita kwa ufafanuzi wa Matumizi ya lugha ya ishara katika nyimbo za Taarabu za Mohamed Ahmed lakini kazi yake imetusaidia katika kuzipata baadhi ya nyimbo na maelezo aliyoyapata kupitia kwenye mahojiano yake na watunzi na baadhi ya waimbaji wa nyimbo za Taarabu Zanzibar.

## 1.3 Kauli ya Tamko la Utafiti

Mohamed Ahmed Moh'd mi mmoja kati ya watunzi wa nyimbo za taarab asilia ambaye kazi zake hazijachunguzwa kwa kiwango kama hiki cha uzamili. Mtunzi huyu ana nyimbo nyingi ambazo zimesheheni matumizi ya lugha ya Ishara kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Kumekuwa na kauli kuwa taarabu asilia hutumia zaidi lugha ya ishara na mafumbo katika kueleza mambo ikilinganishwa na taarabu ya mipasho ambayo hutumia lugha ya wazi inayotajwa kuwa ni kinyume na utamaduni wa jamii ya Waswahili na Waafrika kwa jumla (Khamis, 2013). Hivyo, katika utafiti huu tunachunguza matumizi ya lugha ya ishara katika nyimbo za taarab asilia za mtunzi Mohamed Ahmed Moh'd ili pamoja na

mambo mengine ktuthibitisha kwa vitendo kauli kuwa, “nyimbo za taarabu asilia hutumia zaidi lugha ya ishara ikilinganishwa na nyimbo za taarabu ya mipasho.”

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahususi kama ifuatavyo:

### 1.4.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza lugha ya ishara katika nyimbo za taraab zilizotungwa na Mohammed Ahmed Moh’d.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

i. Kueleza lugha ya ishara iliyotumika katika nyimbo za taraab za mtunzi Mohammed Ahmed Mohd.
ii. Kufafanua maana ya lugha ya ishara iliyotumika katika nyimbo za Mohammed Ahmed.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

(i) Ni ishara zipi zinazopatikana katika nyimbo za taraab za mtunzi Mohammed Ahmed?
(ii) Ni maana gani zinazopatikana kupitia lugha ishara aliyoitumia mtunzi Mohammed Ahmed Mohd katika nyimbo zake?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Kumalizika kwa utafiti huu kutakuwa ni zao la kuzielewa nyimbo zilizotungwa na mtunzi Mohammed Ahmed Mohd. Halikadhalika utafiti huu utawasaidia watunzi wachanga katika kuitumia vyema lugha ya ishara katika utunzi wa nyimbo zao ili

kukuza maadili na utamaduni wa watanzania. Hata hivyo utafiti huu utawasaidia wasomi, wahadhiri, walimu na wanafunzi katika kutumia kwenye kazi zao kama marejeleo ya kazi zao ili kufikia kwenye malengo yao. Mwisho utafiti huu utatumika katika kuhifadhi na kukuza Matumizi yanadharia ya simiotiki katika kufafanua lugha ya ishara na misamiati yake iliyotumika katika nyimbo hizo za mtunzi Mohammed Ahmed Mohd.

## 1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kufanyika katika kisiwa cha unguja katika mkoa wa mjini magharibi ‘A’ na ‘B’. Maeneo yaliyochaguliwa katika mkoa wa mjini magharibi ‘A’ni Michenzani,Kikwajuni na Mwembetanga.uteuzi wa maeneo haya umekuja kutokana na kupatikana kwa wapenzi na mashabiki wa Taarabu asilia.vilevile maeneo haya hususan Michenzani ndipo anapoishi mtunzi wetu na ndipo panapo maskani yake kubwa.kwa upande wa mjini Magharibi ‘B’mtafiti anatarajia kulitumia eneo la Tomondo kwasababu ndipo anapopatikana mkurugenzi wa kikundi cha Zanzibar One ambae anazitumia baadhi ya nyimbo za mtunzi huyu katika shughuli na sherehe mbalimbali.

## 1.8 Mpangilio wa Tasinifu

Utafiti huu umejengeka katika sura tano ambapo sura ya kwanza itaanza na utangulizi wa jumla wa utafiti na usuli wa utafiti ambao utaeleza chimbuko na historia ya maada ikiwemo na historia ya mtunzi. Sehemu hii pia itatoa kauli ya utafiti na kutoa malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, maswali ya utafiti, mipaka na mawanda ya utafiti.

Sura ya pili imefafanua na kuonesha mapitio na machapisho ya kazi tangulizi zilizohusiana na mada yetu pamoja na ufafanuzi wa lugha ya fasihi, taswira na lugha ya ishara katika fasihi. Nadharia ya utafiti ambapo kwa mujibu wa mada yetu tumetumia nadharia ya Simiotiki iliyofafanuliwa na wataalamu kadhaa na kuelezwa chimbuko na mawanda ya nadharia hii na vipi imetusaidia katika kazi hii. Sura ya tatu imejiegemeza zaidi katika mbinu mbalimbali zitakazo tumika katika kukusanyia data. Sura ya nne ni uwasilishaji na uchambuzi wa data. Sura ya tano hitimisho la utafiti, mapendekezo, viambatishi na marejeleo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imeanza kwa kupitia maandishi yaliyowahi kuzungumzia fasihi na lugha kwa ujumla wake. Katika kueleza hayo itafafanua mitazamo iliyoelezwa na wanafasihi juu ya umuhimu wa lugha katika uchambuzi wa matini za kifasihi na lugha ya ushairi. Vilevile sura hii itaangalia mitazamo ya wataalamu juu ya maana ya taswira na ufafanuzi wa taswira na lugha ya ishara katika kazi za fasihi pamoja na kuzipitia kazi tangulizi zilizojikita katika nyimbo za aina tofauti zikiwemo nyimbo za taarab. Mbali na hayo sura hii itafafanua nadharia ya simiotiki kama ilivyofafanuliwa na wataalamu mbalimbali katika kuichambua lugha ya ishara. Nadharia hii ya simiotiki ndiyo itakayotumika katika kuchambua matumizi ya lugha ya ishara yaliyotumika katika nyimbo za Taarab za Mohammed Ahmed Mohammed.

## 2.2 Ufafanuzi wa Dhana Mbalimbali

Katika sehemu hii tumefafanua dhana mbalimbali kama ifuatavyo:

### 2.2.1 Fasihi na Lugha

Wamitila (2008) katika Fasihi na lugha amezungumza kuwa lugha ni nyenzo kuu katika Fasihi na kwa mhakiki hivyo ni muhimu kuitambua nafasi hii kubwa. Katika maandishi yake A. Richerds alibainisha Matumizi mawili makuu kwa kutofautisha kati ya “lugha ya kisayansi” au lugha ya kirejelezi na “lugha ya kishairi” lugha hisia. Aina ya kwanza ni lugha ambayo kimsingi hutumiwa kwa nia ya urejelezi tu bali ya kuacha athari nyengine ya kinyume chake ni aina ya pili ambayo huwacha athari au hisia fulani kwa anaeisoma.

Hii ni aina ya lugha ambayo inahusishwa kwa kiasi kikubwa na lugha inayopatikana katika matini za kifasihi. Wanafasihi wanatambua umuhimu wa lugha katika uchambuzi wa matini za kifasihi. Taaluma inayotumika katika uchambuzi wa lugha katika Fasihi inayofahamika kama uhakiki wa kiisimu au taaluma mitindo. Ingawa katika kitabu chake hauzungumzia lugha ya ishara katika nyimbo za Mohammed Ahmed lakini ametoa ufafanuzi wa kinadharia unaotolewa na mawazo yanayotolewa na wahakiki wananadharia mbalimbali kuhusu suala hili la kuwepo au kutokuwepo kwa lugha ya kifasihi. Lengo hasa la kulichunguza suala hili si kuparaganya taaluma ya fasiihi kama ambavyo inajulikana bali ni kusisitiza kuwa mtunzi au mwandishi anachotaka kuwa kwenye hazina pana ya ubunifu. Ikiwa tutaifunga lugha kwa kusema kuwa ipo lugha maalumu ya kifasihi tutaishia kubana uhuru alionao mwamndishi kwa kudokeza kuwa mtunzi asieitumia lugha hiyo si mtunzi mzuri.

Msingi hasa wa Fasihi ni uhuru wa muandishi wa kuweza kuchota hazina pana, mawasiliano ya kifasihi hayajengwi kwenye msingi wa kuwepo kwa msimbo maalumu wa kiisimu au kilugha bali ni kule kutokuwepo kwa msimbo huo. Suala la lugha ya Fasihi au sifa ya kiisimu ya lugha inayohusishwa na Fasihi limechukuwa nafasi muhimu tangu Nadharia za zamani na hasa Nadharia ya urasimu wa kirusi. Wanaurasimu hawa walisema kuwa lugha ya kifasihi inatofautiana na lugha ya kawaida kwa kuwa zipo mbinu za kuiajinabisha lugha hii, kuifanya ijitokeze na kuifanya tofauti na jinsi lugha ya kawaida ilivyo. Walishikilia kuwa mbinu ya uwajinabishaji inachangia kuwafanya wasomaji wa Fasihi wautambue “ugeni” Fulani wa lugha hiyo. Vile vile kazi hii itatusaidia katika utafiti wetu kutokana na kugusia kipengele cha lugha katika ushairi. Wamitila (2008) anaendelea kueleza

kuwa sifa ya uwajinabishaji inahusishwa zaidi na ushairi ambao kutokana na kaida na kanuni za kimuundo lugha inyotumiwa inaweza kuonekana tofauti na lugha ya kila siku. Si ajabu kuwa wanaurasimu walishikilia zana hii hasa kwa vile walijihusisha kwa kiasi kikubwa na ushairi. Aidha lugha inayopatika katika matini au kazi za kifasihi ni toleo la uteuzi anaoufanya muandishi au mtunzi wa kazi inayohusika. Uteuzi huu unadhibitiwa kwa kiasi kikubwa na malengo ya kimawasiliano na kisanii ya mtunzi maalumu. Suala la uteuzi wa lugha hujitokeza kwa njia iliyowazi zaid katika utanzu wa ushairi. Ushairi huchukuliwa kama tokeo la matumizi ya lugha kwa njia maalumu. Hata hivyo, hii haina maana kuwa uteuzi wa aina hii haupatikani katika nathari, zipo riwaya nyingi ambazo zinaakisi mitindo ya lugha inayohusishwa na ushairi.

### 2.2.2 Nyimbo na Harusi

Msokile (1992) amezungumzia nyimbo na ushairi, ametoa maana ya nyimbo na kueleza majukumu ya nyimbo kazi hii itatusaidia kupata maana ya nyimbo ambayo tutaitumia katika utafiti wetu. Freuchen (1962) ambae amenukuliwa na Msokile (1992) ametoa maana ya nyimbo na kueleza vipi jamii inatoa nyimbo. Maelezo yake yatasaidia katika ufafanuzi wa nyimbo ambazo tutazitumia kwenye utafiti wetu, Mdungi (2007) ameandika juu ya nyimbo za singa rimbwa katika jamii ya watumbatu. Katika utafititi wake amefafanua kuwa nyimbo za singarimbwa zinazoimbwa ndani ya jamii ya watumbatu na mafunzo yake yanavohusiana na jamii hiyo hii inatokana na sababu kwamba nyimbo hizo zinatokana na asili ya kitumbatu na zina husisha zaidi maisha ya wanajamii hao. Kama vile kuzungumzia umuhimu wa kupata kizazi katika familia na kusaidia kwa hali na mali, pia nyimbo hizi

zinazungumzia mambo ya kiuchumi. Tasnifu hii itatusaidia katika ufafanuzi wa nyimbo za taraab za mohammed ahmed ambazo kupitia lugha ya ishara zimeiakisi jamii husika.

Juma (2008) ameandika juu ya nafasi ya nyimbo za unyago katika jamii ya wazanzibari katika zama za utandawazi. Katika tasnifu yake amezungumzia kuhusu nyimbo za unyago ambazo huonesha furaha ya kutoka tabaka moja la kijamii hadi jengine. Nyimbo hizi pia humsisitiza mwanamwali majukumu yajayo ya utuuzima na kuuwaga utoto katika utafiti wetu tasnifu hii itatusaidia katika kufafanua utumikaji wa ishara zinazopelekea kuonesha hali za huzuni, furaha, majonzi unaojitokeza katika nyimbo za Mohammed Ahmed Moh'd.

Nae Hassan (2007) katika utafiti wake amechunguza athari za nyimbo katika maisha ya mke na mume katika kijiji cha jambiani. Katika kazi yake hiyo amegundua kuwa msanja hivi sasa hausikani katika ndoa nyingi, lakini inaonekana kuwa wanajamii hao wa kusini unguja bado wanakubaliana kuwa nyimbo za msanja ni kama msingi wa maisha ya ndoa. Kazi hii ya tasnifu imetusaidia zaidi katika kufafanua ishara zilizozungumzia mapenzi ya ndoa katika nyimbo za Mohmmed Ahmed Mohd.

Thabit (2007) katika tasnifu yake amejadili nafasi ya nyimbo za taraab katika jamii ya wazanzibari wa leo katika utafiti wake amejiegemeza zaidi katika kuichambua nafasi ya taarab katika jamii ya wazanzibari na wala sio vipengele vyengine vilivyomo katika sanaa ya taarab. Katika tasnifu hii imetupatia maana ya nyimbo ambayo amemnukuu msokile na kutoa ufafanuzi kuhusu nyimbo ambayo pia

alimnukuu Freuch. Hivyo kazi hii imetusadia kupata muelekeo wa ufafanuzi wa nyimbo za taarabu na mifano ya nyimbo hizo.

Chama cha waandhishi wa vitabu kanda ya Zanzibar (2007) wameandika baadhi ya historia fupi za watunzi wa mashairi ya Zanzibar na baadhi mashairi yao, katika kitabu hiki kitatusaidia katika kupata historia za watunzi wa mashairi ambayo yameimbwa katika vikundi vya taarabu vya zanizibar miongoni mwa watunzi hao ni bwana Mohammed Ahmed Moh'd na mashairi yake mengi yameimbwa na NAAD AKHWAAN SWAFAA

Mulokozi (1975) katika andiko lake alilozungumzia nyimbo za watoto anasema kuwa ingawa nyimbo hizo zinaimbwa na watoto wakijifurahisha, zinabeba ujumbe muhimu katika kuyaongoza mawazo yao katika maswala muhimu yahusuyo jamii yao. Anafafanua kuwa, ni vigumu sana kuelewa asili ya kila wimbo kwani kama zilivyo tanzu nyengine za Fasihi simulizi,nyimbo za watoto huibuka na kubadilika kutokana na wakati na mazingira ingawa katika kazi yake hakugusia suala la nyimbo za taarabu lakini kazi hii itatusaidia kwa vile amezungumzia nyimbo na dhima yake kwa jamii.

Nae Ndulute (1977) kwa upande wake anazichukulia kuwa nyimbo za watoto ni zile zinazoimbwa na watoto wakiwa shuleni au katika michezo yao ya kila siku,anasema kuwa watoto wanapokuwa katika michezo yao huimba nyimbo ambazo huzikumbuka hata wanapokuwa watuwazima,kutokana na kazi hii kuzungumzia nyimbo imetusaidia katika ufafanuzi wa nyimbo tutakazozitumia katika tasnifu yetu.

Balisidya (1987) ameziangalia nyimbo za watoto wa Kiswahili kwa kukiri kuwepo kwa nyimbo hizo katika jamii. Katika kazi yake Balisidya anasema kuwa nyimbo za watoto zimekuwepo katika jamii tangu zamani, na zimekuwa zikiimbwa zikipokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mawazo haya hayana tofauti na ya Mulokozi (1975) ila yanatusaidia kubaini kwamba nyimbo za watoto zinarithishwa kutoka kizazi hadi kingine. Vile vile yanashadidia kwamba, jamii ikibadilika basi hata na nyimbo za watoto katika jamii hiyo hubadilika. Kazi hii imetusaidia katika kuzifafanua lugha za ishara zilizotumika katika nyimbo za Taarab zinavyoiakisi jamii.

Mbarouk (1981) katika utafiti wake wa nyimbo za michezo ya watoto amegundua kuwa ni burudani kwa watoto na hutumia lugha rahisi yenye kueleka na aghalabu isiyokuwa na tamathali za semi. Mbarouk anasistiza kwamba nyimbo hizi ziimbwe kwa kuzingatia Matumizi ya lugha ya Kiswahili bila ya shaka mbarouk alishatishwa na Matumizi makubwa ya lugha ya kiingereza katika nyimbo za Kiswahili na kasumba kwamba kujua kiingereza ndio kustaarabika. Mbarouk anaibuka na mawazo kwamba mafunzo na ujumbe uliomo katika nyimbo hizo huwafikia watoto kwa haraka zaidi kwa kutumia lugha yao halisi. Mawazo ya Mbarouk (1981) yanakaziwa na Rwilomba aliyetafiti Matumizi ya sanaa za maonesho katika njia ya kufundisha masomo ya hisabati na kiingereza katika shule za awali na msingi Rwilomba aligundua kuwa nyimbo za watoto za Kiswahili zina mchango mkubwa katika kutolea maarifa ya masomo mengine kwa watoto. Hivyo hoja za wataalamu hawa zimetusaidia katika utafiti wetu kutokana na kuhusisha umuhimu wa nyimbo katika kutoa mafunzo kwa jamii.

Msokile (1992) anaendelea kufafanua kwamba kwa kawaida nyimbo za watoto za Kiswahili huongelea mazingira wanayoishi na kucheza watoto na kwamba ina dhima kubwa. Hapa msokile anasistiza kuwa kusambazwa kwa nyimbo hizo kutoka kizazi kimoja hadi kingine kunasababisha mabadiliko ya nyimba sambamba na mabadiliko ya jamii, hivyo kutokana na ufafanuzi wake kazi yake imetusaidia katika ufafanuzi wa ishara ndani ya nyimbo za taarab na jinsi zinavyoongelea mazingira halisi ya jamii.

Senkoro (1996) anaangalia nyimbo za kubembeleza watoto yaani bembezi na anaeleza jinsi nyimbo hizo zinavyoakisi masuala ya kijnsia na uhalisi wa maisha katika jamii, anasema kuwa nyimbo hizi hutumiwa kuelezea mitazamo ya wabembelezaji kuhusu, ndoa na waume. Pia huelezea hofu, malalamiko, uchungu, hasira na matumaini yao. Anasistiza kuwa katika jamii za mfumo jike kama zile za wakaguru nyimbo hizi zinaonesha umuhimu wa kijamii wa mwanamke kama kiumbe huru anaeshiriki sawa na kikamilifu katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Senkoro anaendelea kusema kuwa bembezi kutoka pwani ya afrika ya mashariki ambapo mfumo wa kikabaila na dume umejikita zinaonesha picha ya utumwa, umaskini na ukosaji wa haki za kijamii, kazi hii ya senkoro imetusaidia sana katika utafiti wetu kutokana na kugusia kwake jinsi nyimbo zinavyoakisi masuala ya kijinsia na uhalisia wa maisha katika jamii kitu ambacho tutuakifafanua kupitia lugha ya ishara aliyotumia mtunzi mohammrd ahmed katika nyimbo zake za taarab.

Omari (2008) amechunguza nyimbo za watoto kwa kutilia mkazo namna watoto wanavochorwa na kushirikishwa kimajukumu katika mukhtadha wa kumjenga kiakili

na kimatendo. Katika uchambuzi huo anatuangazia kwamba kuna haja ya kuzisikilza nyimbo hizi kwa kuwa mbali na kutoa burudani hubeba ujumbe unaohitaji kuchambuliwa kitaalam. Mawazo yake yanatusukuma kuzichambua baadhi ya nyimbo za watoto za Kiswahili na kubainisha jinsi zinavopitisha ujumbe murua kwa jamii zinazosikiliza nyimbo hizo kupitia uchambuzi wa kazi yake imetusadia katika utafiti wetu wakati wa kuchunguza lugha ya ishara iliyotumika katika nyimbo za taarab za mohammed ahmed inavyoichora na kuishirikisha jamii katika Nyanja zote za maisha.

Khatib (2014) katika kitabu chake ameeleza asili ya taarab Zanzibar, taarab katika vipindi mbalimbali vya maisha ambapo amefafanua kukua na kuenea kwa taarab, ingawa hakujikita katika kufafanua Matumizi ya lugha za ishara katika nyimbo zake, kazi yake imetusaidia kuzipata baadhi ya nyimbo na maelezo aliyoyapata katika mahojiano yake na watunzi na baadhi ya waimbaji wa nyimbo za taarab za Zanzibar.

Khatib (1981) anaeleza kwamba nyimbo ni lazima zifungamane na ushairi simulizi, pia nyimbo huwa na kawaida ya kueleza hisia nzito zilizomo katika jamii Fulani, nyimbo zikiwemo zile za taarab lazima zifanane na jamii husika kulingana na wakati na mahitaji ya jamii. Hivyo maudhui yake yaowane na maisha ya jamii. Hasa utamaduni wa jamii husika kazi hii itatusaidia sana katika utafiti wetu kwani miongoni mwa nyimbo zilizozungumziwa zimetungwa na mtunzi huyu Mohammed Ahmed Moh’d ambazo tumezitolea ufafanuzi katika tasnifu yetu.

Chama cha Wandishi wa Vitabu Kanda ya Zanzibar (2007) wametoa baadhi ya historia fupi za watunzi wa mashairi wa Zanzibar na mashairi yao huku wakielezea

na historia fupi za watunzi hao miongoni mwa watunzi hao ni msanii wa maigizo wa Zanzibar bwana chimbeni kheri, marehemu bakari abedi. Mbali ya watunzi wa nyimbo vilevile kuna baadhi ya watunzi wa mashairi ya kawaida tu, ingawa kitabu hiki hakikuzungumzia Matumizi ya lugha za ishara katika nyimbo za taarab lakini kimeeleza historia fupi ya bwana Mohammed Ahmed Moh’d na baadhi ya nyimbo zake ambazo tutazitumia katika utafiti wetu.

Naye Steven (2012) anaelezea majukumu na athari za nyimbo za watoto katika enzi za Teknologia ya kidijitali, katika makala yake amewanukuu waandishi kama mulokozi (1975) ambaye amezungumzia ujumbe uliomo katika nyimbo za watoto. Ndulute (1977) ambae amechunguza nyimbo za watoto zilizoimbwa katika michezo mbalimbali ingawa hawakugusia suala la matumizi ya lugha za ishara katika nyimbo za taarab lakini makala zao zimetuongoza katika kubaini vionjo vya lugha katika nyimbo na tumefanyia kazi katika tasinifu yetu.

Baraza la Kiswahili Zanzibar (2008) katika makala iliyoandikwa na Bakari Khamis inayozungumzia Kiswahili cha asili cha kina mama wa visiwani Zanzibar, makala ambayo imefafanua nyimbo zinazotumiwa na kina mama wa kizanzibari, katika kipengele hiki ameeleza kuwa akina mama hutumia nyimbo furaha, huzuni, masikitiko au kutokuridhika na hali Fulani. Kupitia nyimbo kina mama huchombeza watoto hufunzia maharusi namna ya kuishi maisha ya ndoa (uk.35) halikadhali ameeleza jinsi wanawake wanavotumia nyimbo za taarab katika kujiliwaza, kujipumbaza, kujibembeleza, kuomba radhi au kuelezea hisia za mapenzi (uk.36) ametoa nyimbo kama:

Hakika nakupenda
Mazoea yana tabu
Kajaomba samahani
Nipepee mpenzi

Katika ufafanuzi wake ingawa hakufafanua juu ya lugha ya ishara katika nyimbo hizo lakini imetusaidia katika kufafanua nyimbo za taarab za Mohammed Ahmed tukazozitumia.

Hamad (2008) katika makala yake aliyoandika katika utamaduni wa mzanzibari amezungumzia Matumizi ya ushairi na muziki wa Kiswahili katika maisha ya kila siku pwani ya afrika mashariki. Katika makala yake ameeleza maana ya ushairi kuwa ni mpangilio maalum wa maneno yenye kuleta mvuto wa aina yake, vilevile ni maneno yenye mpangilio na yenye mahadhi maalum. Kihistoria ushairi ulianza katika mawasiliano kati ya binaadamu na ulitia hima katika kuendelea na kazi za kila siku. Ushairi unachukua muziki kwa yale mahadhi au namna ushairi huo unavyotolewa, kwa kawaida ushairi unaghaniwa na sio kutongolewa au kutambwa kama hadithi. Hivyo, ushairi una hali ya muziki ndani yake. Muziki katika ushairi ni sauti ya wimbo, kinanda, na ngoma (Johnson 1978) katika kazi yake amefafanua nyimbo na ngoma ambazo zinatumiwa na watu wa mwambao wa afrika mashariki hususan katika visiwa vya Zanzibar katika shughuli za kila siku, hata hivyo hakugusia lugha ya ishara iliyomo katika taaarab lakini ufafanuzi wake unaohusiana na Matumizi ya ushairi na muziki utasaidia katika kazi hii kwa kuhusisha utumikaji wa lugha ya ishara katika mashairi ya nyimbo zilizotungwa na mtunzi wetu.

Mbunda (1981) akimnukuu Matteru anaufafanua wimbo kwamba ni “aina ya ushairi unaoimbwa peke yake au kwa kuhusishwa na ngoma au pia na kucheza kwa

muimbaji wake”. Katika kuelezea mpangilio wa nyimbo amesema kuwa nyimbo kwa kawaida hubeba mpangilio au mfuatano maalum wa sauti, mwendo, picha na ishara. Katika jamii mbalimbali nyimbo zimekuwa na dhima anuwai kulingana na umuhimu wake. Matteru katika kuzichunguza nyimbo hasa za Tanzania amezigawa katika makundi matano hivyo dhima za nyimbo hizo hufuata migawanyo hiyo, ameyaorodhesha makundi hayo kama ifuatavyo; Nyimbo za ngoma ambazo maudhui yake ni kufurahisha katika mikutano ama sherehe, nyimbo za jando na unyago na dini, nyimbo za kazi kama vile kuvua, kuwinda, kulima na kusaga, nyimbo za watoto kama zile za kuwabembelezea watoto wakilia na kucheza na nyimbo za jumla ambazo mtu anaweza kujiimbia.

Wamitila (2005) katika wanyama amezibainisha dhima za nyimbo kuwa ni pamoja na kuonyesha uhusiano wa kijamii, kuonyesha migogoro, kejeli, kubembeleza, kuliwaza, kutumbuiza kuongoza na kuburudisha. Aidha nyimbo zina majukumu mengineyo kama vile kuhifadhi na kurikodi matukio muhimu ya kihistoria, kudhihirisha thamani ya utamaduni katika jamii, kuhamasisha jamii kutenda jambo fulani au kuleta mashirikiano, hutumika pia kuelimisha nakupitsha maarifa kadhaa kwa wanajamii. Ufafanuzi huu wa Wamitila (2005) umesaidia katika tasnifu hii kwa kutoa ufafanuzi lugha ya ishara aliyoitumia mtunzi Mohamed Ahmed katika nyimbo zake na jinsi zinavyotoa dhima kwa jamii husika.

Muhammed (2010) Katika tasnifu yake ameeleza mchango wa nyimbo za unyago katika kumkomaza mwari kiunyumba ambapo amefafanua mafunzo kadhaa yanayopatikana katika nyimbo hizo, katika ufafanuzi wake amefafanua taswira zinazojitokeza katika nyimbo na mafunzo ya taswira hizo. Mbali ya kuwa kazi hii

haikujikita katika nyimbo za Taarabu lakini imesaidia katika kufafanua dhamira zinazojitokeza katika nyimbo za taarab kupitia nadharia ya SImiotiki inayoelekeza matokeo ya ishara zinazojikita katika msimbo wa kihemenitiki.

Othman na wenziwe (2015) katika tasnifu yao wamechunguza Taswira zinazopatikana katika nyimbo za mkugo, katika utafiti wao wamejikita zaidi katika kufafanua taashira zinazopatikana katika nyimbo na jinsi zinavyotoa mafunzo yakumfunza mwanajamii.wameeleza kuwa nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii za kiafrika.Utanzu huu wa Fasihi simulizi hutumika kuburudisha, kuonya, kufunza, kuarifu, kunogeshahadithi, kuomboleza, kuliwaza, kubembeleza mtoto, kutia hamasa katika kazi au vitani nakadhalika. Mkugo ni moja wapo ya ngoma maarufu sana katika jamii ya kaskazini Unguja ipigwapo nyimbo hii huambatana na nyimbo maarufu sana katika jamii ya kaskazini Unguja, kupitia tasnifu hii ingawa haikuzungumzia nyimbo za taarab za mtunzi wetu lakini imesaidia kwa kiasi kikubwa katika kufafanua taswira zilizotokana na lugha ya ishara zinazotoa maana mbili tofauti katika nyimbo za taraab zilizotungwa na mtunzi Mohammed Ahmed zinazoibua picha halisi za maisha ya jamii.

## 2.3 Taswira na Lugha ya Ishara katika Fasihi

Haji na wenzake (1983) amezungumzia sanaa ilyomo katika vitendawili katika ufafanuzi wake amezungumzia Matumizi ya lugha ya ishara yaliyomo katika vitendawili. Katika makala yake amefafanua vitendawili vitano na kueleza lugha ya ishara iliyotumika katika vitendawili hivyo kwa Mfano; mgeni wangu kila niendapo namkuta (nzi) ameeleza lugha ya ishara iliyotumika ni neno mgeni limeashiria nzi. Nzi amepewa na kunasibishwana mgeni kutokana na kuona kuwa hana nasabu na

wale wanaoishi kwenye nyumba. Ingawa katika kitabu hiki waandishi hawa hawakuzungumzia nyimbo za taarab za Mohammed Ahmed lakini imetusaidia katika kutoa ufafanuzi wa lugha ya ishara alilyoitumika katika nyimbo hizo kupitia ufafanuzi uliotolewa katika lugha ya ishara iliyotumika katika lugha ya vitendawili kwa mujibu wa waandishi wake.

Wamitila (2008) anaeleza maana ya taswira kuwa ni tamathali ya usemi ambapo jina au neno linalohusishwa na kitu Fulani linatumiwa kusimamia kitu kamili au kinachohusishwa nacho. Si ajabu kutumia neno “jembe” kusimamia au kurejelea kilimo au mkulima (Wamitila, 2008). Matumizi ya taswira hupatikana kwa wingi si tu katika matini za kifasihi bali pia katika lugha ya maongezi ya kila siku. Katika ukurasa wa 365-366 anaelezea jazanda kuwa ni neno ambalo hutumiwa kurejelea ile hali ya kutumia picha ua taswira katika kazi ya kifasihi. Jazanda hutokana na Matumizi ya lugha, maelezo ya msimulizi au mwandhishi pamoja na Matumizi ya tamathali za usemi. Kuwepo kwa tamathali kama tashibihi au sitiari kuna uwezo wa kuunda taswira au picha katika kazi inayohusika. Ingawa hakugusia suala la nyimbo za taarab katika maelezo yake, lakini kazi hii imetusaidia katika kutoa ufafanuzi wa taswira zilizotoa picha katika nyimbo zilizotumika katika kazi hii kwa kueleza dhamira za picha hizo.

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2016) katika makala ya jahazi (uk88 -89) Mdungi ameeleza katika makala ya matumizi ya tamathali za semi na vipengele vyengine vya lugha baina ya Muyaka wa Muhaji na Shaaban Robert amezungumzia lugha ya ishara katika baadhi ya tamathali za semi katika maelezo yake amesema ishara ni aina ya tamathali za semi ambayo aghalabu hutumika pamoja na sitiari au hutumika

na kinaya. Sitiari inahusisha; ishara inaashiria kitu Fulani na kukipima kama tulivyoona katika mfano wa “Mfalme, Ali simba au ni simba yaani simba huashiria kiongozi mkali, katili au mwenye tabia ya umangimeza na sitiari hutumika kuhusisha au kuonesha uhusiano uliokuwepo kati ya mfalme na simba.”

Matumizi ya ishara ni jambo moja la maana katika ushairi ambapo washairi hutumia ishara ili kufumba na kuwafanya watu wengine wasifahamu kisemwacho kwa hivyo, Matumizi ya ishara yanaweza kulifanya shairi lisifahamike kwa watu wengi. Katika matumizi ya picha, lugha ya kawaida na msamiati unaofahamika kikawaida lakini kueleza hisi tofauti na zile tuzipatazo wakati tunalisoma shairi juu juu” (Gibbe 1980).

Mbwenne mwinda na na t’aza kuenemewa ni tomezi
Mno vikanishangaza hapatwa na makuuzi
Hafikiri nikiwaza mola ndie muwawazi
Tui na mani na mbuzi, huvushwaje dau moja? Abdul-azizi (1979-92).

Katika ubeti huu tunaona umejengwa na picha au taswira ambayo inawachora wanyama, “tui na mani na mbuzi” wanaovushwa katika dau hali hawapatani na kila mmoja ana nguvu na ushujaa. Pia mtunzi ameijenga sitiari kupitia wanyama hao ambao wamehusishwa na watu wenye kisasi wanaoishi mahali pamoja.

Mara nyingi taswira huambatana na Matumizi ya tamathali za semi hasa sitiari na tashbiha, katika taswira tunagundua matumizi ya ishara mbali mbali zinazowakilisha mawazo, dhana, vitu au mtu anaendelea kusema kuwa taswira ni lugha inayochora picha ya vitu au mahali kwa  kutumia ishara katika taswira tunagundua maelezo jinsi yanavyopangwa na msanii huweza kufanya hadhira izipate aina mbalimbali za hisi

zinazoshughulikiwa na kazi ihusikayo na Fasihi yaani hisi za kunusa, kuona, kusikia, kuonja na kugusa (Senkoro, 2011).

## 2.4 Mkabala wa Kinadharia

Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Simiotiki ambayo imeweza kusaidia katika kuchanganua matumizi ya lugha ya ishara katika nyimbo za taarab zilizotungwa na Mohammed Ahmed Moh'd sababu za kutumia nadharia ya Simiotiki kutokana na nadharia hii kuwa imesadifu zaidi kwa vile imezungumzia kwa upana sana juu ya vipengele vya lugha ya ishara na uashiriaji katika kazi za fasihi,vile vile imesadifu katika kumsaidia mtafiti kuchambua na kuzifafanua data kwa kuzieleza picha na ishara zilizotumika ziliashiria kitu au jambo fulani ambavyo ndio kiini cha utafiti huu**.** Kuna mambo mengi yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya semiotiki na bado mjadala unaohusiana na ufafanuzi wa nadharia hii ungalipo. Hivyo kupitia nadharia hii utafiti huu umejikita zaidi katika kufafanua matumizi ya lugha ya ishara katika nyimbo za taarab za mtunzi Mohammed Ahmed Moh'd. Eco (1976) alieleza kuwa semiotiki inahusishwa na kila kitu ambacho kinaweza kuchukuliwa kuwa ishara. Katika kazi hii imerejelea baadhi ya mawazo ya wanasemiotiki kwa mujibu wa wataalamu na waandishi mbalimbali ambao wameifafanua nadharia hii na kuyataja matawi na vipera vyake.

Wataalamu na waandishi mbalimbali wa masuala ya kiisimu, kipragmatiki na kifasihi wametoa fafanuzi tofautitofauti za semiotiki. Baadhi ya fafanuzi hizi ni:

Massamba (2004:76) alieleza kuwa, Simiotiki ni taaluma ya kisayansi inayojishughulisha na uchunguzi na uchanganuzi wa mifumo ya ishara mbalimbali

ikiwa inazingatia zaidi uhusiano baina ya kiwakilishi na kiwakilishwa. Maelezo haya yanaelekea kuoana na maelezo ya Ferdinand de Saussure (1946) ya kiashirii na kiashiriwa ambayo yamezingatiwa kwa kiasi kikubwa katika kuchanganua matumizi ya ishara katika nyimbo za taarab za mtunzi Mohammed Ahmed Moh'd.

Nao Wafula na Njogu (2007:103) walieleza Simiotiki kama taaluma ya mipangilio ya ishara inayomwezesha binadamu kuona vitu au hali kama ishara zenye maana. Hata hivyo, ni muhimu kuelewa kwamba, semiotiki hasa hujishughulisha na masuala ya ishara kiupana, matumizi ya ishara na matumizi ya lugha kwa jumla katika kazi za kifasihi. Wataalamu hawa wanasisitiza kuwa semiotiki huzungumzia uashiriaji wa vipashio vya lugha au tamathali ilhali nadharia ya umuundo inahusu namna ishara zinavyowekwa katika utaratibu unaoziwezesha kufahamika. Jambo muhimu linalojitokeza katika fasiri hizi ni kwamba, semiotiki ni mfumo wa ishara ambazo zinawakilisha kitu au maana fulani.

Wamitila (2003:190) alieleza kuwa, Simiotiki ni aina ya nadharia ya kimuundo inayojishughulisha na ishara na maana za ishara hizo katika kazi za kifasihi. Semiotiki huangazia uashiriaji na jinsi kazi za kifasihi zinavyowasiliana na wasomaji. Nadharia hii aidha huchunguza kwa nini kazi za kifasihi zina maana zilizo nazo kwa wasomaji wa kazi hizo.

Selden (1985:85) alieleza kuwa neno'Simiotiki' limenyambuliwa kutokana na neno la Kigiriki 'semeion' lenye maana ya ishara linalowakilisha vikundi vya wafuasi wa mielekeo fulani. Naye Wamitila (2002:132) alieleza kwamba ' semiotiki' ni neno la lugha ya Kiyunani (Kigiriki) lenye maana ya ishara na ambalo linatumiwa kuelezea


mielekeo ya makundi fulani ya kihakiki. Wamitila anakubaliana na Selden kuhusu asili ya neno semiotiki kwa kuwarejelea Bailey, Matejk, Steiner ("*The Sign System*: vii") walioeleza kuwa' semiotiki ni mchakato ambapo vitu na matukio huja kutambuliwa kama ishara na kiumbe hai ambacho kinahisi.' Maoni ya Selden ni kuwa semiotiki ni taaluma ambayo hufanya kazi kwenye desturi pana za kiutamaduni zinazohusisha ishara violwa na ishara tajwa. Anapozungumzia semiotiki ya kisasa anasema kuwa inatumiwa kurejelea uwanja unaoendelea kubadilika kwa elimu ya masomo ambayo huangaza fenomena ya maana katika jamii (1985:86 -7).

Tunaweza kusema kuwa mielekeo ya makundi haya ya kiuchambuzi yamezua mtindo wa kuhakiki kazi za kifasihi unaoangazia matumizi ya ishara. Wamitila (2002:132-3) alieleza kuwa kimsingi' Simiotiki ni nadharia inayojishughulisha na ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi.'Kwa sababu ya kupendelea matumizi ya neno 'matini', baadhi ya wananadharia huiita nadharia ya semiotiki 'umatini'. Hata hivyo neno 'semiotiki' kama tulivyoeleza haliwezi kuchukuliwa kwamba ni kisawe cha neno 'umatini'.

### 2.4.1 Mihimili ya Nadharia ya Semiotiki

Wamitila (2002:133) akisisitiza umuhimu wa mihimili ya Simiotiki, alieleza kuwa historia ya semiotiki imefuata mikondo mbalimbali na haiwezekani ikachunguzwa vizuri bila kubaini matapo yaliyoiwekea misingi kuanzia Urasimi wa Kirusi, Shule ya Isimu ya Praque hadi kufikia hatua ya leo inapohusishwa zaidi na wahakiki kama vile Eco, Greimas, Todorov, Kristeva, Derrida na Barthes.

Kuzuka kwa nadharia ya semiotiki kunahusishwa na miaka ya 1970 wakati ambapo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuacha umuundo uliokuwa umeutawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Kulingana na Wamitila (2002:178–9) Saussure alifafanua lugha kama mfumo wa ishara ambazo huangaza na kuunda 'mkufu wa ishara'. Kwa Saussure, kila ishara huwa na sehemu mbili: kiashirii (sauti au wasilisho la kimaandishi) na kiashiriwa (maana ya kiashirii)**.** Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kiashirii ni neno lenyewe na kiashiriwa ni maana yenyewe ya kiashirii. Kwa mujibu wa Saussure, kiashirii ni picha-sauti ilhali kiashiriwa ni dhana. Mchoro ufuatao unaorejelewa na Daniel Chandler katika *Semiotics for Beginners (2002)* unadhihirisha muundo wa ishara wenye sehemu mbili wa Saussure. Katika mchoro huu pana ishara, kiashiriwa na kiashirii.




**Mchoro A: Ishara, kiashiriwa na kiashirii**

**Kutoka: Chandler (2002).**


Kwa hivyo, ishara ni jumla ya matokeo ya uhusiano baina ya kiashirii na kiashiriwa (Saussure 1986:67). Aliitazama Simiotiki kama mfumo wa lugha kiishara ambapo maana huundwa kutokana na elementi hizi mbili. Semiotiki huangalia matini yoyote ile kama iliyosheheni ishara mbalimbali zinazofungamanishwa na maana ya kifasihi. Kwa mfano:

Kiashirii cha neno ‘mbwa’ ni sauti ya kiutamkaji au herufi za kiuandikaji lakini kiashiriwa ni mnyama anayefugwa nyumbani. Msimamo wa Saussure ni kuwa maana za ishara zina uhusiano wa kuzuka kwa nadharia ya semiotiki kunahusishwa na miaka ya 1970 wakati ambapo kulikuwa na mwelekeo mkubwa wa kuuasi na kuuacha umuundo uliokuwa umeutawala uhakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960.

Kulingana na Wamitila (2002: 178–9) Saussure alifafanua lugha kama mfumo wa ishara ambazo huangaza na kuunda ‘mkufu wa ishara’. Kwa Saussure, kila ishara huwa na sehemu mbili: kiashirii (sauti au wasilisho la kimaandishi) na kiashiriwa (maana ya kiashirii)**.** Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kiashirii ni neno lenyewe na kiashiriwa ni maana yenyewe ya kiashirii. Kwa mujibu wa Saussure, kiashirii ni picha-sauti ilhali kiashiriwa ni dhana. Mchoro ufuatao unaorejelewa na Daniel Chandler katika *Semiotics for Beginners (2002)* unadhihirisha muundo Nalo neno ‘mvulana’ linapata maana kutokana na uhusiano uliopo kati yake na ishara nyingine na pia viashirii vingine katika ‘mkufu wa ishara’ kama ‘mzee’, shaibu’ na ‘buda.’ Katika mfano huu, ishara moja hupata maana kutokana na tofauti iliyopo kati yake na ishara nyingine. Wanasemiotiki wanashikilia kuwa, aidha kiashirii huweza kuwa kile kile bali kinachoashiriwa kinaweza kuwa tofauti. Kwa mfano, huko Ulaya, neno ‘pombe’ huweza kuwa ishara ya urafiki, pongezi, wema, ukarimu au mapenzi lakini kiashirii kinabaki kuwa neno ‘mvinyo’. Kwa hivyo, tunaweza kusema kuwa kiashirii kimoja kinakuwa na viashiriwa vingi katika lugha ya kawaida. Maoni haya ya kiashirii na kiashiriwa yanatiliwa mkazo katika kuchanganua matumizi ya ishara katika nyimbo za taarab za mtunzi Mohammed Ahmed Moh’d..

(a) Neno au kiashirii cha 'rangi nyekundu' chaweza kuwa na viashiriwa kama vile hatari, uhai, kizuizi, mapenzi n.k. Mfano huu ni msingi wa matumizi ya polisemia.

Naye mwanafalsafa Peirce anahusishwa na kielezo cha ishara ambacho kina pembe tatu: ishara, yambwa na kifasiri. Mchoro ufuatao umetumiwa kurahisisha uelewaji piramidi ya Peirce inayofafanua ishara.




**Mchoro B: Piramidi ya Peirce ya kufasiri ishara**

**Kutoka:Wamitila (2002:132).**

Peirce aliukubali uchanganuzi wa Saussure wa ishara kuwa na sehemu mbili: kiashirii na kiashiriwa lakini akaongeza sehemu ya tatu – kifasiri. Kwa Peirce, kila ishara huwa na yambwa au kitendwa kinachorejelewa. Wamitila (2002:132) alieleza kifasiri kama kitu kinachochochea katika akili ya anayetafsiri ishara hiyo, yaani ishara ya pili. Kwa mfano, mtu akikuonyesha simba aliyelala mahali fulani, ile ishara ya simba inaweza kulichochea neno 'simba' katika lugha nyingine akilini mwako. Hiki kitakuwa kifasiri. Peirce anasadiki kwamba kila ishara ina misingi inakotegemezwa ili ufasiri wake uwezekane. Anaongeza kuwa misingi hiyo huibua

aina tatu za ishara ambazo ni kielekezi, ishara-tanakali na taashira. Kila mojawapo ya ishara hizi huwa na dhima maalum.

Wamitila (2002:133-4) alifasiri ishara hizi tatu ifuatavyo:

(a) Kielekezi -hutumiwa kufafanua uhusiano fulani baina ya ishara na kinachoashiriwa. Kwa mfano, kicheko kuwa ishara ya kuwepo kwa mtu fulani.

(b) Ishara-tanakali nayo hutumiwa kuonyesha mahali au hali ambapo pana uhusiano kati ya ishara na kiashiriwa. Kwa mfano, picha na michoro ni ishara- tanakali zinazoeleweka. Aidha milio, 'wuuu!' na 'miaoo' ni ishara-tanakali za mbwa na paka mtawalia.


(c) Taashira hueleza aina ya ishara inayoashiria kutegemea matumizi ya kinasibu na kikawaida.

Mawazo ya Peirce ya ishara kutegemezwa kwenye msingi fulani ili kufasiriwa, yaelekea kukubaliana na wazo la Saussure kwamba ishara hazina upekee wa maana isipokuwa zinapofasiriwa katika 'mkufu wa ishara'. Peirce anasifiwa kwa kuhakikisha kuwa nadharia ya Simiotiki haikuishia kuzisambaza sifa za kitaaluma sana kama ulivyofanya umuundo (Wamitila 2002:133).

Wafula na Njogu (2007:103) walieleza kuwa Saussure katika uchanganuzi wake wa Kisimiotiki, aliegemea dhima ya ishara katika jamii ilhali Peirce alishughulikia namna ishara zilivyotumiwa kufafanua vitendo maalum na maana ya ishara hiyo ikitokana na sheria fulani za kiutamaduni, kitanzu na lugha. Chandler (2002: 1)

akizungumzia piramidi ya kisemiotiki ya Peirce, alidhihirisha namna ishara, dhana na kifasiri zilivyounganishwa.

Alifanya hivyo kwa kuhusisha matumizi ya uelewaji, tajriba na kifasiri ili kuonyesha mihusianisho mikuu katika kufasiri ishara kama inavyodhihirika katika mchoro ufuatao:




**Mchoro C: Mihusianisho ya kufasiri ishara.**

**Kutoka: Chandler,D. (2001) *An Introduction to Semiotics)***

Katika piramidi hii ya kisemiotiki:

i. Ishara na dhana huunganishwa na uelewaji wa mtu kuhusu ishara fulani.
ii. Dhana na yambwa huunganishwa na tajriba aliyo nayo mtu kuhusu ishara.
iii. Ishara na yambwa huunganishwa na kanuni au utamaduni wa kikundi cha jamii husika.

Mahusianisho haya ni muhimu katika utafiti wetu kwa kuwa imetusaidia kuelewa namna maana inavyoibuka wakati wa mahusiano ya kila siku na ishara nyingi zilizomo katika mazingira ya kibinadamu.

Peirce alijitokeza na ishara aina tatu: Ishara za ki-ikoni, ishara za kifaharisi na ishara za kitaashira. Ishara za ki-ikoni huwa zina mfanano baina ya ishara na kinachorejelewa(kirejelewa). Hutuelekeza kwenye muktadha au hali halisi na huwa zenye msingi wa kimuhakati. Nazo ishara za kifaharisi huhusisha uhusiano wa kiwakati, kimuktadha au mahali kati ya ishara na kinachotajwa. Huu ni uhusiano halisi, wazi na wa kisababishi. Kwa mfano, hodi mlangoni ni ishara kuwa pana mtu au mlio wa gari kuwa ishara ya kuwepo kwa gari (Hawkes 1977:129). Iwapo msomaji atalielewa neno katika kazi ya kifasihi itamlazimu kuliangalia katika muktadha fulani. Kwa mfano, moshi ni ishara ya kiwakati inayoashiria kuwepo kwa moto.

Ishara za kitaashira nazo, huwa ni tukio la kiutamaduni. Huwa hazina mfanano wa uhusiano kati ya ishara na kiashiriwa bali huwa jambo au kitu cha makubaliano au kikanuni. Kwa mfano, njiwa kutumika kuashiria amani.

Nadharia ya semiotiki haiwezi kukamilika bila kurejelea mawazo ya Roland Barthes kuhusu misimbo mitano ya usomaji ambayo imeacha athari kubwa katika uhakiki wa ishara na uashiriaji katika kazi za kifasihi. Misimbo hii ni miongoni mwa nguzo kuu za nadhharia ya semiotiki. Barthes (1994)anaeleza kwamba kuna aina tano za misimbo zinazotumika katika kazi za fasihi ambazo kwa pamoja huunda nadharia ya semiotiki. Aina hizo ni msimbo wa kimatukio, kihemenitiki, kiseme, kiishara na kiutamaduni.

Msimbo wa kimatukio; msimbo huu unahusu jinsi matukio yanayopatikana katika hadithi au masimulizi yanayofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa

msuko wa kazi hiyo kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavyofuatana kithari au kisababishi. Mtunzi wa kazi ya fasihi huweza kuunda visa na matukio kwa njia ya msimbo wa kimatukio(Solomon,1988)kwa mfano mtunzi wa nyimbo ta taarab ya *lishalo haliji tena* na nyimbo ya *juu ya miba inochoma* ambapo mtunzi anasimulia matukio yaliyompelekea kujuta na kusema lishalo haliruhusu kuja tena vile vile katika wimbo wa pili anasimulia matukio yaliyomfanya ajihisi yuko juu ya miba na sio kwenye raha. Mtunzi ametumia matukio haya ili kuonyesha uhalisia wa maisha ya kimapenzi kwa baadhi ya wapendanao na jinsi wanavyoathiriwa na maisha hayo.

> Msimbo wa kihemenitiki; Msimbo huu unahusu taharuki na usimulizi na kwa hivyo huitwa msimbo wa kusimulia au msimbo wa kutamba hadithi na unatokana na anuani ya kifasihi kama jina la kitabu, jina la shairi kichwa cha igizo, /onyesho, au jina la sura katika riwaya(Mark,19995)kwa mfano shairi la *sasa sinae na kunguru* yanajenga taharuki ya kutaka kujua maudhui yanayopatikana katika nyimbo hizo.

Msimbo wa ki-seme; Neno seme hutumiwa kueleza elementi nasibihi ya kisementiki, Semantiki ni taalima inayoshughulikia maana za maneno katika lugha ya mwanaadamu. Katika taaluma ya semantiki maneno huwa yanakuwa na maana ya msingi na maana ya ziada. Maana ya msingi ni ile ambayo inaweza kutumika na kurejelewa katika muktadha rasmin wakati maana za ziada za maneno zinaweza kutumika katika muktadha usio rasmin. Msimbo wa kiseme katika taaluma ya kifasihi hutumiwa na wanafasihi katika kujenga dhamira na maudhui kwa kutumia maneno ambayo yanatoa ukaribu wa maana ya msingi ya neno na kile kinachorejelewa na neno hilo kifasihi (Wright,1975) kwa mfano,”Said ni simba”ni sitiari yenye nomino mbili, Saidi ni jina la mtu na simba ni jina la mnyama wa porini ambae ni mkali sana kutokana na sifa yake ya kuuwa wanyama wengine kwa ajili ya

chakula na wanaadamu pia, kifasihi Saidi anapewa sifa kwa hivyo, tunapata unasibishi kuwa Saidi ni mkali kwelikweli na hana mchezo na mtu. Katika utafiti wetu tumetumia msimbo huu katika kuchambua matimizi ya lugha ya sitiari, tashbiha, tashhisi na kejeli kama zinavyojitokeza katika nyimbo zetu zilizotungwa na Mohammed Ahmed Moh'd..

Msimbo wa kiishara: Matumizi ya lugha ya ishara yanatumiwa na waandishi wa kazi za fasihi kwa kiasi kikubwa. (Senkoro,2006). Hii inatokana na ukweli kuwa kazi ya fasihi husawiri maisha halisi ya jamii kwa kutumia lugha ya ishara, picha na kisha kuyawasilisha kwa jamii. Msimbo wa kiishara wa nadharia ya simiotiki humsaidia mtafiti au mhakiki wa kazi ya kifasihi kuweza kubainisha lugha ya ishara iliyotumika katika kazi ya fasihi na kuweza kusema kuwa hapa kuna dhamira fulani kwa mfano katika shairi la **ndege wangu** linalosema;

Ndege wangu kaumbika, mzuri asokifani,
Utadhani malaika, anapendeza machoni,

Katulia hana shaka, yumo mwangu mikononi, (Khatib 2014) katika mashairi mbalimbali waimbaji hutumia ndege katika kutoa wasifu wa dhana ya mapenzi na wapendanao mwimbaji humsifu mpenzi wake kwa kutumia picha ya ndege, kama ilivyojitokeza katika shairi letu.

Msimbo wa kiurejelezi: Hujengwa kutokana na viashirii vya kiutamaduni ambavyo vinarejelewa katika kazi za kifasihi. Huhusisha matumizi ya vitu fulani vinavyoeleweka na wasomaji na hivyo kuipa kazi fulani nguzo ya kiutamaduni.

Katika kuashiria mambo haya mtunzi hutumia silka mila desturi na hata imani katika kuiwasilisha kazi yake kama alivyotumia Mohammed Ahmed anaposema;

**Namtafuta Banati**
Namtafuta banati, mwenye jamali ya umbo,
Na mwnye tamu sauti, ilo kwake ndio pambo,
Mwenye mapenzi ya dhati, awe pia ni mrembo.

Awe na njema adabu, vizuri aloleleka,
Asinitie aibu, nyumbani nikimuweka,
Asiwe yeye sababu, ya mimi kutukanika. (Khatib2014 uk 70).

Katika shairi hili mtunzi ametumia vitu kadhaa vinavyoashiria utamaduni na desturi za Watanzania ambao huwa na vigezo vinavyoendana na silka na mila zao katika kuchagua mchumba kama vile adabu nzuri na aloleleka kwa malezi mema.

Wamitila (2002:179) aliendeleza maoni ya Wana-Umuundo kwa kusema kwamba, ishara moja inaweza kuwa na maana nyingi iwapo itawekwa au kukitwa kwenye muktadha wa kijamii na hivyo jamii kuwa na athari kubwa juu ya maana. Hii ina maana kuwa kiashiriwa hakiwezi kuwa funge. Naye mwanaudenguzi Bakhtin alieleza ishara kama kitu kinachotegemea kingine kinachozungumziwa kwa kuwa ishara haina maana funge. Hutegemea usemezano wa msemaji na msemezwa. Mwanariwaya za kiupelelezi Jacques Derrida aliendeleza wazo la Bakhtin kwa kudai kuwa ishara ambayo si funge haina kitovu cha maana ya ishara.

Kutokana na mawazo haya tunaweza kusema kuwa viashiriwa vikikitwa kwenye muktadha wa kimazungumzo huweza kubadilika kutegemea muktadha wa kiusemi na iwapo muktadha utabadilika nayo maana inabadilika. Kwa hiyo, inakuwa vigumu kudai kuwa kuna kitovu maalum cha maana mahali popote pale (Wamitila 2002:179-

180). Wataalamu wa kiuumbuaji, Voloshnov, Bakhtin na Derrida ni wahakiki wa hapo baadaye walioisukuma mbele nadharia ya semiotiki.

**Udhaifu wa nadharia Hii**

Udhaifu mkubwa wa nadharia hii ya simiotiki unatokana na msisitizo wake mkubwa kujiegemeza kwenye lugha na sifa nyengine zinaonekana ndogo badala ya kujihusisha na fasihi kwenye upana wake (Wamitila,2002).

Pamoja na upungufu wake, nadharia hii iliteuliwa kwa sababu mihimili yake mitano ilionekana kufaa katika kutimiza malengo ya utafiti huu. Kwa hiyo katika utafiti huu nadharia ya semiotiki itatumika katika kuchunguza matumizi ya lugha ya ishara aliyoyatumia mtunzi Mohammed Ahmed Mohd katika nyimbo zake za taarab. Nadharia hii inaonekana inafaa katika kuchunguza lugha za kitamathali hizo kama vile sitiari, ishara, mafumbo, taswira nakejeli ili kuweza kubainisha dhamira mbalimbali zilizotumika katika nyimbo hizo.

Kutokana na ufafanuzi uliotolewaa na wataalamu mbalimbali walioijadili nadharia hii ya semiotiki nimeiona inafaa katika kuchunguza kujadili, kufafanua na kuchambua data za utafiti huu. Ili kufikia malengo ya utafiti huu nadharia hii inaonekana kuwa na uthabiti wa kukidhi malengo ya utafiti

## 2.5 Hitimisho

Katika sehemu hii imejumuisha mapitio ya kazi tangulizi ambazo zilisaidia katika kupata maana ya taswira kutoka kwa wataalamu mbalimbali nakupata ufafanuzi wa lugha ya ishara katika kazi za fasihi, na kupitia machapisho na tafiti mbalimbali

zilizohusiana na mada hii. Katika kupitia kazi hizo nimebaini kuwa tafiti nyingi zimezungumzia nyimbo katika maudhui nazo ni nyimbo kwa ujumla hakuna tafiti iliyo zungumzia nyimbo za mtunzi huyu Mohammed Ahmed na utunzi wake. Mbali na hayo katika sehemu hii nimeibainisha nadharia iliyotumika katika kuchunguza, kuchambua na kufafanua data na matokeo ya utafiti, nadharia hiyo nimeifafanua ili iweze kufikia katika malengo ya utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii nitaeleza mbinu ambazo utafiti huu umezitumia katika kukusanyia data na kueleza maeneo ambayo data hizo zimepatikana. Halikadhalika mtafiti amefafanua njia ambazo amezitumia katika kukusanyia taarifa zake, ikiwemo na vifaa alivyovitumia kwa kazi hiyo. Kothari (2008) anaeleza kwamba mbinu za utafiti ni muhimu katika utafiti wa kitaalamu kwa sababu ni kutokana na mbinu hizo ndio utafiti huo wa kitaalamu kisayansi na sio kiubabaishaji. Hivyo sura hii itajadili kuhusu umbo la utafiti, eneo la utafiti, aina za data, mbinu za ukusanyaji, mbinu za uchambuzi wa data na maadili ya utafiti.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ambao kwa wakati mwengine hujulikana kama umbo la utafiti, hutoa picha kamili inayoonyesha namna na jinsi utafiti ulivyofanyika tangu unaanza mpaka unamalizika (Kothari2008) ameeleza kuwa usanifu wa utafiti ndio unaoonyesha kuwa utafiti husika ulikuwa ni wa namna gani na data zilikusanywa vipi. Katika utafiti huu amechunguza nyimbo husika ametumia aina hii kwa kuzichunguza kifani baadhi ya nyimbo zilizotungwa na Mohammed Ahmed Moh'd. (Yin, 1994) anaeleza kuwa uchunguzi kifani kwa jina la kiingereza ni ''case study''ni umbo la utafiti ambalo mtafiti huteua mahali, jambo au kitu maalum ambacho alikishughulikia kwa kina ili kutimiza malengo yake ya utafiti. Utafiti huu umeteua nyimbo za taarab za mtunzi maalum ambazo ndizo zitakazoshughulikiwa kwa kina ili kukamilisha lengo kuu la utafiti.

Robert (2007) anaeleza kuwa uchunguzi kifani ni umbo la utafiti ambalo lina faida nyingi kwa mtafiti. Kwanza umbo hili la utafiti humuwezesha mtafiti kutumia muda wake vizuri kwa kushughulikia jambo ambalo tayari analijua tofauti na kufanya utafiti bila ya kujuwa nini hasa unashughulikia. Katika hali hii mtafiti hatashughulikia nyimbo za taarab tu bali atajikita katika nyimbo zile zilizotungwa na Mohammed Ahmed Mohammed tu. Pili umbo hili la utafiti humsaidia mtafiti kuchunguza jambo kwa kina na kulitolea mahitimisho yanayostahili. Tatu umbo hili limemsaidia mtafiti kutimia gharama ndogo na kupata data nyingi. Hii inatokana na kuwa tayari mtafiti ameshatambua ni kitu gani anachoshughulikia na data zake ni zipi na atazipata wapi na hivyo hatotumia fedha nyingi kutafuta data zisizohitajika.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Kwa upande wa eneo la utafiti huu umefanyika katika eneo la mjini magharibi'A na B Unguja ambapo katika mjini magharibi A ametumia eneo la Michenzani, na Kikwajuni. Hii ni kutokana na kuwa maeneo haya ndipo wanapopatikana wapenzi, waimbaji na mashabiki wengi wa nyimbo za Taaraab akiwemo mtunzi wa nyimbo hizo ambae mwenyewe pia anapatikana katika maeneo haya na makaazi yake halisi ni michenzani jumba namba 7. Ingawa katika maeneo mengine wapo wapenzi wa Taarabu asilia lakini wengi wao ni wapenzi wa nyimbo za CULTURE MUSICAL CLUB na wanaopatikana katika maeneo niliyoyataja wengi wao ni wapenzi wa NAAD AKHWAN SWAFAA ambacho ndicho kikundi alichokitungia nyimbo zake nyingi na ndicho kikundi anachoimbia mtunzi huyu. Mbali na hayo uteuzi wa eneo la Rahaleo katika kituo cha redio ni eneo anapofanya kazi mkurugenzi wa kikundi cha Zanzibar One ambae nae huzitumia nyimbo za mtunzi huyu kuziimba katika

shuughuli mbali mbali za kijamii, kichama na za kiserikali. Eneo la mwisho alilolitumia ni skuli ya kiembe samaki sekondari ambapo mtafiti aliwapata walengwa wake ambao ni walimu na ni mashabiki wa taarabu asilia wengine ni wapenzi wa Culture na wengine ni wapenzi wa Nard ikhwan swafaa.

## 3.4 Kundi Lengwa

Kundi lengwa katika utafiti huu limejumuisha wapenzi, waimbaji na mashabiki wa nyimbo za taarab asilia ambao kwa upande wa vijana ni kuanzia umri wa miaka 30-45 na wazee ni kati ya miaka 46-na kuendelea.

### 3.4.1 Sampuli na Usampulishaji

Sampuli iliyotumika katika utafiti huu ni sampuli ya wakaazi wa Unguja mjini katika mkoa wa mjini Magharib A na ambapo makundi lengwa yanatokea katika maeneo tuliyoyaainisha hapo awali. Mtafiti katika uteuzi huu alichagua wazee wenye umri wa miaka 50 na kuendelea na kwa upande wa vijana uliwashirikisha vijana kati ya miaka 35-49, uteuzi wa kundi lengwa la namna hii umetokana na uhalisia wa jamii yenyewe unaothibitishwa kwamba wapenzi na mashabiki wa Taarabu asilia Zanzibar ni watu wenye kuanzia umri wa miaka 35 na kuendelea ambao ni wenye kuijua asili na mvuto wa Taarabu ni watu wenye rika la kuanzia miaka 49 na kuendelea ambao wanaishi katika maeneo niliyoyateua hasa katika mkoa wa mjini magharibi A ambako mashabiki wake wanahudhuria ghafla na shughuli mbalimbali za Taarabu. Utafiti ulikuwa na Jumla ya watafitiwa 40 ambapo wazee walikuwa 10, vijana 10, waimbaji 10 na mashabiki 10 ambapo suala la jinsia lilizingatiwa.

## 3.5 Aina ya Data Zilizokusanywa

Katika utafiti huu data za aina mbili zimeweza kukusanywa nazo ni data za msingi na data za upili.

### 3.5.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hujulikana kama data halisi ambazo hazijawahi kukusanywa na mtunzi mwengine kwa minajili utafiti kama huo anaokusudia kuufanya (Goods1966). Data za msingi huwa ni ghafi na hukusanywa kwa lengo la kuziba pengo la utafiti liloachwa na watafiti wengine waliotangulia (Kombo naTromph, 2006) Data za msingi katika utafiti huu data hizi zilikusanywa kutoka katika nyimbo halisi zilizotungwa na mtunzi Mohammed Ahmed Moh'd. Nyimbo hizo mtafiti alizipata kutoka kwa mtunzi mwenyewe na baadhi alizipata kupitia kwa waimbaji waliotungiwa na kuimba.

### 3.5.2 Mbinu za Kukusanyia Data za Msingi

Data za msingi zilikusanywa kwa kutumia zaidi maktaba na kumtumia mtunzi mwenyewe, ambapo mtafiti alianza kuzipitia kazi tangulizi na machapisho yaliyozungumzia taarab Zanzibar na kufanikiwa kuzipata baadhi ya nyimbo zilizotungwa na mtunzi huyu. Vilevile, mtunzi alimpatia mtafiti baadhi ya vitabu na rekodi zake alizoziandika nyimbo zake. Mbinu ya usaili pia ilitumika katika kukusanya data ambapo tuliwasaili wazee, vijana, waimbaji na mashabiki wa taarabu kuhusiana na masuala mbalimbali yaliyotusaidia kupata data za utafiti.

### 3.5.3 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zimekusanywa na kuchapishwa katika vitabu, makala, tasinifu, majarida, magazeti na katika wavuti na tovuti. Data hizi hukusanywa kwa lengo la kupata data za ziada ambazo husaidia katika kushadadia hoja. Data hizi hukusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji wa nyaraka. (Robson, 2007) anaeleza kuwa upitiaji wa nyaraka ni mbinu ya kukusanya data za utafiti kwa mtafiti kusoma machapisho katika maktaba na kuchukuwa kile anachokihitaji kulingana na mada yake ya utafiti. Hivyo, data za upili zilikusanywa kupitia maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

## 3.6 Uchambuzi wa Data

Mbinu iliyotumika katika utafiti huu ni mbinu ya kimaelezo. John (2007) anasema kwamba uchunguzi wa kimaelezo ni mbinu inayomruhusu mtafiti kusikiliza au kuona au kusoma kazi ya kifasihi ikiwemo nyimbo na tamthilia, kisha kueleza maudhui ambayo yamebeba dhamira, falsafa, migogoro, ujumbe na mtazamo/msimamo wa mtunzi. Katika kufanya hivyo pia mtafiti ataelewa matumizi ya lugha, wahusika mtindo, muundo na mandhari katika kazi anayoisoma, kuisikia au kuitazama. Nae Kothari (2009) anaeleza kuwa mkabala usiokuwa wa kiidadi unaleta na kuzalisha matokeo yasiyoonyesha idadi au kiasi na unalenga kutoa maelezzo zaidi. Enon na White (2000) kama walivyonukuliwa na Kileo (2011) wanaeleza kuwa mkabala usiokuwa wakiidadi ni njia ya maelezo na data zinazokusanywa haziwasilishwi kwa njia ya kitakwimu. Sababu za kuchagua mkabala huu ni kutokana na mada inayofanyiwa utafiti si ya kimahesabu, hivyo haihitaji kufanyiwa mahesabu.

Katika kufanikisha uchambuzi wa data katika utafiti huu kwaza mtafiti alizisoma na kuzipitia kwa kina nyimbo zote nilizoziteua ili kupata data za utafiti. Data zilipatikana katika uteuzi wa misamiati, beti, majina ya mashairi husika na sentensi katika ushairi wa nyimbo husika. Baada ya hapo kupitia data hizo zitachambuliwa na kutolewa maelezo kulingana na nadharia iliyoteuliwa ambayo ni nadharia ya semiotiki kulingana na mahitaji ya mada yanahusiana na malengo makuu yanayojibu maswala ya utafiti wetu.

## 3.7 Hitimisho

Sura hii imefafanua juu ya mbinu zilizotumika katika utafiti huu na kutoa umbo halisi la utafiti linaloonyesha namna utafiti huu ulivyofanyika. Mbali na hayo sura hii imeeleza maeneo ambayo utafiti huu umefanyika na sababu za kuteua maeneo hayo sehemu hii pia imetufafanulia juu ya uteuzi wa kundi lengwa na aina ya data zilizokusanywa kupitia kundi hilo na kutoa aina ya data zilizokusanywa na mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data hizo na kueleza jinsi zilivyochambuliwa. Vilevile sura hii imeeleza vifaa vilivyotumika katika utafiti huu kuhitimisha kwa kutoa sampuli ya utafiti na kuona jinsi utakavyokuwa.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Tasinifu hii ililenga kutimiza malengo mahususi ya utafiti ambayo yalikuwa ni kuainisha nyimbo za taarab za mtunzi Mohamed Ahmed Moh'd na kisha kufafanua matumizi ya lugha ya ishara katika nyimbo hizo. Kutokana na ukaribu wa kimantiki wa malengo haya mahususi tumeona ni vema tukafanya uchambuzi kwa kuyaunganisha. Tumeanza kwa kuainisha wimbo husika baada ya kuibainisha tukafanya ufafanuzi wake kwa maana ya kuonyesha lugha ya ishara iliyotumika.

## 4.2 Uainishaji wa Nyimbo na Ufafanuzi wa Lugha ya Ishara

Katika sehemu hii tumeainisha nyimbo za taarab za mtunzi mteule na kisha tukafafanua matumizi ya ishara yaliyopo katika nyimbo husika.

### 4.2.1 Wimbo wa Kwanza: KIBIRITI NA PETROLI

*Kibiriti na petroli iwapo umeiweka,*
*Hivi ni vitu viwili visije kukutanika,*
*Kusalimika muhali lazima pataripuka,*
*Bora uvitenge mbali hapo utasalimika.*

*Katu haviwi salama jambo hili ni hakika,*
*Moto kuja ni lazima na wala hapana shaka,*
*Tena tabu kuuzima moto ukishakuwaka,*
*Moto wake ni nakama lazima kukhasirika.*

*Katu usiiamini japo kwa moja dakika,*
*Kabisa havipatani mara moja huripuka,*
*Utakuwa khatarini huwezi kunusurika,*
*Na jambo hili yakini wengi limeshawafika.*
*KIITIKO;*
*Pamoja ukiviweka hiyo ni khiari yako,*
*Muhali kusalimika utazuka mlipuko.*

Lugha iliyotumika katika wiimbo huu ni lugha iliyosheheni ishara ambapo imefumbwa kwa msimbo wa kimatukio na msimbo wa kiishara. Kwa kuangalia juu ya msimbo wa kimatukio unapatikana kupitia usimulizi wa matukio yanayoweza kusababishwa na kuwepo pamoja kwa kibiriti na petrol kama unavyofafanua ubeti wa kwanza na wapili ambao ubeti wa kwanza unaeleza vitu hivi jinsi vilivyotofauti, na ubeti wa pili unajenga taharuki ya jinsi tukio la hatari linavyoweza kupatikana kwa kuwepo pamoja kwa vitu viwili hivi ambapo msanii anatupa picha ya kuzuka kwa moto ambao kuzimika kwake ni tabu sana. Picha hii tunaipata pale anaposema;

Moto kuja ni lazima na wala hapana shaka
Tena tabu kuuzima moto ukisha kuwaka
Moto wake ni nakama lazima kukhasirika

Kwa upande wa msimbo wa kiishara wimbo huu umetumia Kibiriti na Petroli kuashiria jamii juu ya athari ya mchanganyiko wa jinsia mbili katika jamii. Kwa mujibu wa Senkoro (2006) Matumizi ya lugha ishara yanatumiwa na waandishi wa kazi za fasihi kwa kiwango kikubwa. Hii inatokana na ukweli kuwa, kazi ya fasihi husawiri maisha halisi ya jamii kwa kutumia lugha ya picha na ishara na kisha huyawasilisha kwa jamii kwa kuiangalia nadharia ya simiontiki inatusaidia kuuhakiki wimbo huu kwa kuweza kutoa dhamira zilizojitokeza kupitia ishara hii ya kiberiti na petroli. Msanii ametumia vitu hivi kutoa dhamira ya mporomoko wa maadili ambapo kupitia ubeti wa kwanza anaonyesha jinsi vitu viwili vilivyokuwa haramu kuviweka faragha anasema;

Kibiriti na petroli Iwapo umeviweka,
Hivi ni vitu viwili visije kukutanika,
Kusalimika muhali lazima pataripuka,

Katika ubeti huu ametumia kibiriti na petrol kuashiria jinsia mbili na kufafanua kua hivi ni vitu viwili tofauti havifai kukutanishwa faragha. Endapo jamii itaviweka pammoja bila ya hadhari yoyote hapana usalama kwasababu patatokezea fitna itakayozusha balaa la maharibiko kati ya mke na mume lazima wataathiriana.

Katika kutilia mkazo kwake Mtunzi anaonyesha kuwa Kibiriti ni ishara ya kichocheo ambacho kikikutana na petrol kinaripua jamii nzima. Ishara hii imesadifu katika kuiangalia jinsi ya kike na ya kiume moja inaweza kua kichocheo cha maovu kwa jinsia ya pili hivyo vikiwa pamoja vinaondosha usalama, furaha, mafahamiano, maelewano na muelekeo mwema wa jamii na ndio maana Mtunzi katika ubeti wa pili akasema:

Moto kuja ni lazima na wala hapana shaka,
Tena tabu kuuzima moto ukishakuwaka,
Moto wake ni nakama lazima kukhasirika.

Hapa Mohd Ahmed anatuonyesha jinsi athari kubwa inavyoikumba jamii kwa kuvikutanisha vitu viwili hivi bila ya tahadhari kwani jinsia hizi zinavyoathiriana uhasama na athari kubwa hufika kwa jamii nzima kwani haitasahaulika milele.

### 4.2.2 Wimbo wa Pili: NANASI

*Nanasi uzuri wake wanipendeza machoni,*
*Naipenda ladha yake nilitiapo kinywani,*
*Ajabu utamu wake linapendeza moyoni.*

*Ukiliona nanasi Limetulia duakni,*
*Bei yake ni rahisi Si ghali ni wastani,*
*Kama unayo nafasi Nunua ule nyumbani.*

*Ununue liwe lako Lisiwe ni la Fulani,*
*Liwe lako mali yako Uwe nalo mikononi,*
*Lako wewe peke yako Ule unapotamani.*

*Usije kulivamia Chagua lenye thamani,*
*Nanasi lisilopea Halina ladha kinywani,*
*Utakuja lichukia Tamu yake huioni.*

*KIITIKIO;*
*Asiyekula nanasi Hajala kitu kitamu.*

Matumizi ya lugha ya ishara yaliyojitokeza katika nyimbo hii yamaejikita katika msimbo wa kiseme, msimbno wa kiishara na msimbo wa kihementiki. Hali hii imejitokeza kuptia uteuzi wa neno NANASI ambalo kwa mujibu wa (Wright, 1975) anafafanua msimbo wa kiseme kwa kuhusisha na semantiki na kusema semantiki ni taaluma inayoshughulikia maana za maneno katika lugha za Mwanaadamu. Katika taaluma ya semantiki maneno huwa na maana ya msingi na maana ya ziada. Maana ya msingi ya neno ni ile ambayo inaweza kutumika na kurejelewa katika muktadha rasmin wakati maana za ziada za neno zinaweza kurejelewa katika muktadha usio rasmin, Katika mtazamo huu neno nanasi tunaweza tukalieleza limetumika katika maana mbili tofauti, maana ya kwanza ya nanasi ni tunda halisi la nanasi lenye sifa ya utamu kama Mtunzi alivyoeleza na maana ya pili ya nanasi ni maana ya ziada ambayo inaashiria mwanamke mzuri wa kuishi na mume. Kwa upande wa maana hii ya ziada ubeti wa kwanza tunaona jinsi Mtunzi alivyomsifu mwanamke alipomuona ansema:

*Nanasi uzuri wake Wanipendeza machoni,*
*Naipenda ladha yake Nilitiapo kinywani,*
*Ajabu utamu wake Linapendeza moyoni.*

Katika ubeti wa pili Mtunzi anaonyesha maeneo anayopatikana mwanamke mzuri, anaelekeza kua mwanamke mzuri ni yule aliyetunzwa kwao kwa ulinzi na malezi imara, na hapatikani kirahisi ni lazima uonane na mwenye duka, muelewane bei ili

awe wako wa milele. Hapa Mtunzi anatutanabahisha kuwa hawafaidi wale wanokula ovyo majiani ila walao ni wale wanaokula kwa utulivu nyumbani, hali hii tunaipata katika ubeti wa pili anapomalizia kwa kuteua maneno “Nunua ule nyumbani”

Kama unayo nafasi  Nunua ule nyumbani

Katika ubeti wa tatu mtunzi anatoa faida ya kununa nanasi lako na kusema kuwa ili ufaidike na utamu wa nanasi ununuwe lako mali yako na hapo utaweza kulila kwa kadri utakapolitamani. Mwisho mtunzi anamalizia kwa kutoa tahadhari katika uchaguzi wa nanasi lililo bora kwa kutumia sifa tatu muhimu ambazo ni thamani, ladha na utamu ambapo anasisitiza kwa kusema ….Usije kulivamia  Chagua lenye thamani,

Nanasi lisilopeya  Halina ladha kinywani,
Utakuja lichukiya  Tamu yake huioni.

Mbali na hayo nyimbo hii imetumia ishara yenye msimbo wa kihementiki kwa kutumia jina la shairi NANASI ambalo linatoa picha halisi ya tunda la Nanasi lililopea na kuiva vyema. Msanii katika utunzi wake wa nyimbo ametuchorea picha za namna tatu za nanasi ambazo tunazipata kupitia katika beti zake nne za nyimbo hii, katika ubeti wa kwanza ametumia neno Nanasi na kulieleza katika umbo la nje na umbo la ndani la Nanasi ambalo analinasibisha na sifa za mwanamke aliyempenda. Katika ubeti wa pili neno Nanasi linatoa sifa za nanasi zuri na jinsi ya kulipata ambapo imeunganisha na ubeti wa tatu unaotoa ilani jinsi ya kulitunza ili uridhike nalo. Picha ya tatu ya Nanasi ni lile Nanasi lisilofaa ambalo linafafanuliwa

kupitia neno Nanasi alilotumia katika ubeti wa nne ambalo analitolea tahadhari kwa wachaguzi wawe makini katika kupata lile linalofaa ili wafaidike.

Kupitia picha tatu hizi zilizopatikana katika beti za nyimbo hii tunapata dhamira kuu za utunzi wake, ambazo ni kueleza jamii jinsi ya kuzitambua sifa za mwanamke wa kuwachagua kwa ajili ya ndoa ambapo ubeti wa kwanza anaelezo muonekano wa mwanamke na tabia zake zinavyowapendeza watu. Ubeti wa pili na wa tatu mwanamke mzuri ni yule aliyetunzwa kwao kwa heshima na taadhima na asie mzururaji. Vile vile unapomchagua usiwe na lengo la kumchezea ila uwe na nia thabiti ya kumuweka awe wako. Ubeti wa nne anaieleza jamii inapochagua mwanamke ichague yule aliyekuwa tayari kiumri kuolewa na asiwe mdogo aliyekuwa hajafikia umri wa kuolewa na kupevuka kwa kufanya hivyo tunaharibu ladha ya ndoa.

### 4.2.3 Wimbo wa Tatu: NAMPENDA KUMWAMBIA SIWEZI

*Kwa mapenzi nnakonda Moyoni nnaumia,*
*Kuna mtu nampenda Daima anisumbua,*
*Jambo moja lanishinda Siri yangu kumwambia.*

*Nimuonapo machoni Sikitiko hunijia,*
*Majonzi tele moyoni Hakika nateketea,*
*Sijui nifanye nini Hata aweze kujua.*

*Na mdomo hufunngika Maneno hunipotea,*
*Aibu huja nifika Hilo nnalichellea,*
*Ntakuja fedheheka Ataponikatalia.*

*Siri unaibaini Sina budi kuitoa,*
*Naitoa hadharani Ili apate tambua,*
*Sinayo shaka moyoni Mwenyewe anajijua.*

Katika nyimbo hii lugha kuu ya ishara iliyotumika imejiingiza zaidi katika msimbo wa kimatukio ambapo msimbo huu unahusiana na masimulizi Fulani yanayofuatana na jinsi msomaji anavyounda na kuelewa msuko wa kazi hii kwa kuangalia jinsi matukio hayo yanavofuatana na kuathiriana. Mtunzi wa kazi ya fasihi huweza kuunda visa na matukio kwa njia ya msimbo wa kimatukio (Solomon 1988). Mtunzi wa nyimbo hii anaanza kwa kusimulia hisia zake za mapenzi juu ya mtu aliyempenda ambapo katika ubeti wa kwanza anaeleza jinsi moyo wake unavyoumia kwa mtu huyo. Katika ubeti wa pili anaeleza tukio la kumuona mtu huyo na hisia anazozipata, athari kubwa anayoipata endapo akitokea kumuona, lakini kinachosikitisha zaidi ni pale anaposhindwa kusema nae mtu huyo kama anavyoeleza kwa kusema

Majonzi tele moyoni      Hakika nateketea,
Sijuwi nifanye nini        Hata aweze kujua.

Katika usimuliaji wake wake wa mkasa wa mapenzi unavyomuathiri katika ubeti wa tatu tunapata picha ya jinsi alivyonywea kwa unyonge na alivyoganda kwa kufadhaika. Hali hii inajidhihirisha anaposema;

Na mdomo hufungika      Maneno hunipotea,
Aibu kuja nifika              Hilo nalichelea,
Nitakuja fedheheka         Ataponikatalia.

Mwisho anamalizia kwa kueleza kuwa yote yaliyotokea mwanzoni aliona yawe siri kwanza lakini kutokana na anavyoteketea anaona aieleze hadharani ili apate kufikiriwa, kwani ana hakika ishara alizomuonesha mwenyewe anajijua. Masimulizi ya mkasa huu wa mapenzi yanafafanua kwamba anaependa anateketea na mapenzi ila kusema anashindwa.

Kwa mujibu wa msimbo huu wa masimulizi wa matukio ambao umetoa pia dhamira ya nyimbo hii kulingana na matukio yaliyopangwa katika beti tunaona unalenga kwenye athari ya mapenzi ya upande mmoja, ambapo anaependa anaposhindwa kujieleza kwa ampendae, mapenzi humuathiri yeye mwenyewe na kushindwa kujua la kufanya.

### 4.2.4 Wimbo wa 4: KUNGURU

*Kunguru ndege laghai* *Unatabu kumnasa,*
*Kama yeye hatokei* *Mwenye hila na mikasa,*
*Japo ukifanya rai* *Weka mbele kumkosa.*

*Anasifika kwa woga* *Mwepesi wa kuepuka,*
*Ukitaka kumtega* *Mgumu kuhadaika,*
*Hutowahi kumpiga* *Mara moja anaruka.*

*Katu humu duniani* *Hapana alomueka,*
*Kunguru hapatikani* *Mjanja wa kusifika,*
*Nitumie hila gani* *Kunguru unamtaka.*

*KIITIKIO*
*Kunguru ndege laghai* *Ana tabu kumnasa*.

Wimbo huu umetumia ishara yenye msimbo wa kiseme, msimbo wa kiishara.Tukianza na msimbo wa kiseme ambapo utumiaji wake wa neno Kunguru unatupa maana mbili, maana ya msingi na maana ya ziada. Kimsingi neno kunguru ni ndege maarufu sana visiwani Zanzibar ambaye ana ila sana ya woga lakini mwenye kupenda kula vitu vya watu (Khatib 2014) Hivyo tunaweza kusema kuwa Kunguru ni ndege mjanja ambae ana tabu kumpata, kama anavyomueleza mtunzi katika ubeti wa kwanza anaposema;

Kunguru ndege laghai Ana tabu kumpata
Kama yeye hatokei Mwenye hila na mikasa
Japo ukifanya rai Weka mbele kumkosa

Hii ni maana ya kwanza ya kunguru ambayo inanasibisha na sifa za ndege mwenyewe halisi. Hata hivyo katika maana ya ziada kunguru tunainasibisha na mtu hasa mwanamke ambae ana msimamo wa kutopatikana kirahisi na mwanaume mwenye uchu wa mapenzi. Mtunzi ametumia sifa za kunguru kama anavyozieleza katika ubeti wa pili ambapo ni moga, hategeki, si rahisi kumpiga, hahadaiki kirahisi. Kupitia maana ya ziada iliyotumika ya kunguru imezifananisha sifa hizi za kunguru na sifa za mwanamke anaemueleza mtunzi.

Katika ubeti wa mwisho mtunzi anaiuliza hadhira njia gani ili ampate kunguru aliemuona. Hii imetudhihirishia wazi kwamba mtunzi amemnasibisha kunguru ndege na mwanamke ambae ana sifa hizo za kunguru.

Hata hivyo, nyimbo hii imetumia msimbo wa kiishara kwa kutumia jina la nyimbo hii kuwa ni kunguru. Kupitia jina hili tunapata taharuki ya kutaka kujua nini amekifanya kunguru. Kutokana na kuzijua sifa za kunguru tunapoliona jina la wimbo tunajenga picha ya ndege huyu na sifa zake.

### 4.2.5 Wimbo wa 5: KANIKIMBIA

*Hasidi kanikimbia* — *Kaniacha nateseka*
*Wapi alipokwendea* — *Sipajuwi kwa hakika*
*Msiba kaniachia* — *Maisha nitakumbuka*

*Hasidi huyu katili* — *Kuniua alitaka*
*Alinitoa akili* — *Nikakonda kwa mashaka*
*Daima alinidhili* — *Bila ya mimi kutaka*

*Hasidi alinitesa* — *Na huku akinicheka*
*Kanimaliza na pesa* — *Sasa nishafilisika*
*Ndipo akafanya visa* — *Upesi kuniepuka*

*Hasidi huyu wenzangu* *Heri alipoondoka*
*Kaninyonya damu yangu* *Hali nikadhoofika*
*Hiyo ni salama yangu* *Mauti yangenifika*

*KIITIKIO*
*Sasa ameshanitoka* *Hasidi wa roho yangu*

Katika nyimbo hii lugha iliyotumika imetoa ishara yenye msimbo wa kimatukio, kiishara na kihemenitiki ambapo katika msimbo wa kimatukio unaeleza tukio zima la kukimbia kwa mpenzi aliyejidai mapenzi ambayo kwa hakika ni ya uongo. Mtunzi anasimulia tukio hilo katika ubeti wa kwanza analieleza tukio hilo la kukimbiwa na aliyekuwa mpenzi wake tukio ambalo limejengwa na picha ya taharuki pale aliposema;

Wapi alipokwendea sipajui kwa hakika
Msiba kaniwachia maisha nitakumbuka

Katika ubeti wa pili mtunzi anasimulia ukatili aliofanyiwa na aliyekuwa mpenzi wake, ukatili ambao ulimtoa akili na kukonda kwa kufanya kila aliloamriwa kufanya bila ya ridhaa yake kama anavyotuonyesha;

Hasidi huyu katili kuniua alitaka
Alinitoa akili nikakonda kwa mashaka
Daima alinidhili bila ya mimi kutaka

Katika ubeti wa tatu na wa nne anaeleza visa na matukio aliyofanyiwa mpaka kufikia kuchoshwa na kufikia hatua ya kutengana miongoni mwa visa hivyo ni kumtesa, kummaliza na pesa.

Katika ubeti wa nne anaeleza mwisho wa maisha yao ulifuatiwa na tukio la kukimbiwa na hasidi huyo ambapo kwa upande wake anaona hiyo ilikuwa ndio nafuu ya usalama wa maisha yake kama anvyosimulia;

Hasidi huyu wenzangu heri alipoondoka
Kaninyonya damu yangu hali nikadhoofika
Hiyo ni salama kwangu mauti yangenifika.

Kupitia msimbo wa kiseme neno hasidi linatoa maana mbili tofauti maana ya kwanza ni mtu mwenye kuhusudu (tafsiri yangu) kupitia maana hii ameipata kutokana na vitendo alivyofanyiwa na aliyekuwa mwandani wake hivyo baada ya kufanyiwa vituko ambavyo havifai mtu na mpenzi wake kufanyiana ndipo alipogundua kuwa huyu si mpenzi bali ni hasidi, na maana ya ziada ni kinyume cha mpenzi wake kuwa alikuwa ni adui aliyetaka kumtoa roho yake kama alivyoeleza katika ubeti wa nne. Kutokana na uteuzi wa jina kanikimbia linatoa ishara ya tukio la kukimbiwa kama inavyojitokeza katika msimbo wa kihemenitiki uliojikita katika kutoa dhima ya utunzi wa nyimbo hii ambayo ni kuieleza jamii juu ya kuwa waangalifu katika kuazisha mahusianona kuwa makini na wapenzi wao.

### 4.2.6 Wimbo wa 6: NILIKUCHAGUA

*Ni bure jeuri yako kwako sitoshughulika,*
*Usidhani peke yako jamali uloumbika,*
*Wameenea wenzako wazuri wakusifika.*

*Sitishwi na sura yako mwishowe itachujuka,*
*Ungekuwa peke yako kiasi ungezuzuka,*
*Lakini wengine wako kwa hili sitosumbuka.*

*Sitojirahisi kwako wala sitobabaika,*
*Iwapo sipendwi kwako kwengine nitapendeka,*
*Duniani wengi wako tachagua nnotaka.*

*KIITIKIO*
*Nimekuchagua wewe* *mimi nawe tupendane*
*Usiponipenda wewe* *watanipenda wengine*.

Katika wimbo huu matumizi makuu ya lugha ya ishara yamejitokeza katika msimbo wa kimatukio ambapo tunaona jinsi mtunzi anaposimulia uzuri wa mpenzi wake ulivyomuhadaa na jinsi alivyoamua kutengana nao hii inajitokeza kuanzia ubeti wa kwanza anaposema;

Nibure jeuri yako kwako sitoshughulika,
Usidhani peke yako jamali uloumbika,
Wameenea wenzako wazuri wakusifika.

Mtunzi anasimulia kisa cha kuachana na mpenzi wake kutokana na jeuri aliyokuwa nayo. Kupitia msimbo wa kihemenitiki, ambao unatokana na anuani ya kifasihi kama jina, hivyo uteuzi wa jina la NILIKUCHAGUA unaashiria kuchoshwa kwa vitendo vya ukatili wa mapenzi na ndio maana mtunzi akatumia kitendo kilichopita NILIKUCHAGUA kuonyesha kuwa hapo awali ndo alimchagua alipokuwa hajamjua tabia yake lakini kwa sasa anamkana. Uteuzi huu umepelekea kusimulia matukio ya tabia zilizomchosha kama anavyotuonyesha katika ubeti wa kwanza na wapili ambapo anaamua kumueleza ukweli;

Sitwishwi na sura yako mwishowe itachujuka,
Ungekuwa peke yako kiasi ungezuzuka,
Lakini wengine wako kwa hili sitosumbuka.

Dhima kuu ya kutumia msimbo wa kihemenitiki na msimbo wa kimatukio ni kuashiria kwa kufichua tabia za dharau zinazozoweleka kwa baadhi ya wanajamii kutokana na kujiona wao ni bora zaidi na wanamvuto wa hali ya juu kuliko wengine kitu ambacho kinakiuka maadili na nidhamu ya malezi.

### 4.2.7 Wimbo wa 7: KISEBUSEBU

*Wajidai hunitaki Wenzio kuwasifia,*
*Kunisengenya huchoki Maovu kunizulia,*
*Kumbe una taharuki Namate kunimezea.*

*Kila tunapokutana Uso unanikunjia,*
*Unajidai kununa Nione wanichukia,*
*Wajifanya haja huna Kumbe unaangamia.*

*Wafanya kisebusebu Mapenzi kuyachezea,*
*Pendo ushaliharibu Moyoni lishapotea,*
*Ikufike na aibu Usije kunililia.*

*Waumwa ndani kwa ndani Na huku wavumilia,*
*Nimekwisha kubaini Moyo wako waumia,*
*Wajikaza kisabuni Nahuku wateketea.*

*KIITIKIO*
*Wafanya kisebusebu Na kiroho kiko papo.*

Mohammed Ahmed katika utunzi wa nyimbo hii ametumia lugha yenye ishara ya msimbo wa kimatukio na msimbo wa kihemenitiki na msimbo wa kihemenitiki ambapo katika usimuliaji wake ameielezea tabia aliyokuwa nayo mpenzi wake ambayo kwake ameiita kama ni kisebusebu. Hali hii inadhihirisha wazi dhamira ya kutojiamini katika maamuzi tabia ambayo alikuwa nayo kutokana na uteuzi wa maneno kama wajidai, unajidai, unajifanya na mwisho ametumia neno wajikaza kisabuni kuonyesha kule kukubali kwake na kukataa kunakopelekea kuonekana kuwa antabia ya kisebusebu. Katika ubeti wa kwanza anaeleza alivyokuwa akikataliwa na kusingiziwa maovu ili aonekane ni mtu mbaya.

Wajidai hunitaki Wenzio kuwasifia,
Kunisengenya hutaki Maovu kunizulia,
Kumbe unataharuki Na mate kunimezea.

Msimbo huu wa kimatukio unaeleza matukio yanayomkumba katika kila hatua ya maisha yao wawili hawa kwa mfano kukunjiwa uso, kununiwa na kupuuzwa hata hivyo mtunzi anaonyesha kuwa yote haya ni matokeo ya kujifanya tu na si ya ukweli au hayatoki moyoni na ndio maana akatumia neno kisebusebu katika kudhihirisha haya ubeti wa nne unathibitisha kwa kusema;

Waumwa ndani kwa ndani Na huku wavumilia,
Nimekwisha kubaini Moyo wako waumia,
Wajikaza kisabuni Na huku wateketea.

### 4.2.8 Wimbo wa 8: SIKUJUA KAMA MAPENZI MATAMU

*Nihakika sikujua Kwamba mapenzi matamu,*
*Si dhihaka nakwambia Yamenitia wazimu,*
*Hivi sasa nakwambia Kwamba yamenilazimu,*
*Kila nikifikiria Inazidi yangu hamu.*

*Tafadhali nipe raha Na raha zote zitimu,*
*Unipe kila furaha zile unozifahamu,*
*Nitononoke kwa siha kwa yale utonikimu,*
*Wala sifanye mzaha mwenzio nimadhulumu.*

*Raha zote za dunia Nipe ukitabasamu,*
*Bila ya kunibania Watu wote wafahamu,*
*Yale yanonivutia Yote usiyakasimu,*
*Mwenzio ninaumia Sina akili timamu.*

*KIITIKIO*
*Hapo mwanzo sikujua ndio kwanza nifahamu,*
*Sasa nimeshatambua kwamba mapenzi matamu.*

Katika wimbo huu mtunzi ametumia msimbo wa kimatukio ambapo amesimulia mambo aliyofanyiwa na kupelekea kukiri kuwa ameonyeshwa utamu wa mapenzi. Hivyo anasisitiza kuwa aongezwe raha alizoonjeshwa hapo awali kama mtunzi anapotusimulia katika ubeti wa pili anaposema;

Tafadhali nipe raha     Na raha zote zitimu,
Unipe kila furaha     Zile unozifahamu,
Nitononoke kwa siha     Kwa yale utonikimu,
Wala sifanye mzaha     Mwenzio nimadhulumu

Katika masimulizi yake amejenga ishara ya msisitizo kwa kulitumia neno RAHA mara tatu katika nyimbo hii. Dhamira kuu inayopatikana ni kuthibitisha na kukiri kuwa mapenzi ni matamu.

### 4.2.9 Wimbo wa 9: LISHALO HALIJI TENA

*Si kwa ngumi wala fimbo     Lishalo haliji tena,*
*Siwezi kula makombo     Japo yawe yamenona,*
*Usiyarejeshe mambo     Yalopita mwaka jana.*
*Uganga na uganguzi     Fanya ukifanya tena,*
*Miti shamba na hirizi     Ule ukiitafuna,*
*Lakini kwako siwezi     Kurudi kudanganyana.*

*Kile nilokitapika     Haramu kuramba tena,*
*Ni basi nimetosheka     Yatosha niloyaona,*
*Ni bora kukuepuka     Siharibu langu jina.*

*Lishalo limeshakwisha     Laleo sio la jana,*
*Siwezi kubahatisha     Wala hamu sina tena,*
*Donda ulonitonesha     Naapa halitapona.*

Mtunzi katika wimbo huu ametumia msimbo wa kiishara ambapo uteuzi wake wa maneno kama fimbo katika ubeti wa kwanza mapambano au mapigano. Kuonyesha kwake mapambano kunalenga jamii ambayo inayomzunguka na kwa kiasi kikubwa mambo haya yanapatikana katika mahusiano na yanaonekana kushamiri kadri siku zinavyozidi kwenda mbele. Msisitizo aliouonyesha msanii ni huu unatoa picha ya kuwa amejidhatiti kwa msimamo wake hata ikibidi kupambana bado msimamo wake ni uleule wa kutorejesha mahusiano. Mbali na hayo mtunzi ametumia neno makombo kuashiria chakula kilicholiwa na kubakia ambacho kwake mtunzi hawezi kukila tena, kupitia msimbo huu wa kiishara tunaona picha aliyoichora mtunzi

inayoonyesha kutosheka kwake na mahusiano hayo kwake yameshakuwa makombo na hivyo hata iweje hawezi kuyarudia kama anavyosema;

Si kwangumi wala fimbo    Lishalo haliji tena,
Siwezi kula makombo    Japo yawe yamenona,
Usiyarejeshe mambo    Yalopita mwaka jana.

Kwa upande wa msimbo wa kiutamaduni mtunzi ameutumia katika kuchora picha ya desturi na silka zinazoendelezwa na watu wa Zanzibar, ambazo ni kushiriki katika tiba za kijadi. Hali hii imedhihirika kutokana na kutumia maneno kama uganga, na uganguzi, miti shamba na hirizi, maneno hayo yanaashiria kuhangaika katika kutafuta tiba ya kurejesha mahusiano hata kufika kwa waganga lakini kutokana msimamo aliouonesha inaonekana kuwa kurudi katika mahusiano hayo ni vigumu. Katika kutumia msimbo wa kimatukio Mohammed Ahmed ameutumia msimbo huu katika utunzi wake kwa kusimulia kiishara matukio ambayo yanakataa mahusiano ya wawili waliopendana na jinsi maamuzi yake yalivyofikia kikomo kwa kusisitiza kuwa hawezi kurejea makombo hata kama yamenona. Kama inavyojitokeza katika ubeti wa kwanza hapo juu. Katika ubeti wa pili Mohammed Ahmed anasimulia tukio zima la kwenda kwa waganga na kutujengea picha ya kutumia tiba ya asili ya mizizi ya kunywa na kutafuna. Katika usimulizi wake tunapata dhamira ya jitihada kutaka kurejesha mapenzi yaliyokwisha zinaweza kufanywa kwa hali na mali lakini mapenzi yasirudi kama mtunzi anavyosimulia;

Uganga na uganguzi    Fanya ukifanya tena,
Mitishamba na hirizi    Ule ukiitafuna,
Lakini kwako siwezi    Kurudi kudanganyana.

Mbali na yote yaliyofanywa kama ni juhudi za kuyarejesha mapenzi zinashindikana na kugonga mwamba na kuonyesha msimamo upo pale pale kama anavyosimulia katika ubeti wa tatu

Kile nilokitapika Haramu kuramba tena,
Nibasi nimetosheka Yatosha niloyaona,
Ni bora kukuepuka Si haribu langu jina.

Msanii anatumia msimbo wa kihemenitiki ambapo anatumia jina la shairi kutoa dhima aliyoikusudia. Jina hili la LISHALO HALIJI TENA linatupa ufupisho wa shairi zima na kiashiria kwamba jambo lolote linapofikia mwisho wake haliwezi kurudi tena.

### 4.2.10 Wimbo wa 10: NDEGE KARUKA KARUDI

*Ndege mzuri ajabu Alitua kitaluni,*
*Mwenye rangi ya dhahabu Na sauti ya kughani,*
*Kumtega tajaribu Nimchukue nyumbani.*

*Mitego nikatumia Nikaiweka mtini,*
*Na mara akaingia Akanasa mtegoni,*
*Mwenyewe akaridhia Nikamtia tunduni.*

*Akatokea hasidi Ndege akamtamani,*
*Akafanya ufisadi Kumtorosha tunduni,*
*Mimi sikutaradidi Kumfuata mwituni.*

*Mwenyewe leo karudi Yumo mwangu mikononi,*
Amenipa na ahadi Ataishi kwa Amani.

Mtunzi ametumia ishara ya msimbo wa kiseme, msimbo wa kimatukio na msimbo wa kiishara ambapo tukichunguza katika msimbo wa kiseme umetumika katika uteuzi wa neno Ndege na neno Mtego. Katika mtazamo wa kiseme katika ishara maneno haya yanatoa maana mbili tofauti maana halisi na ya ziada, maana halisi neno ndege ni aina ya mnyama ambae anaweza kupaa anatumia mabawa. Kwa

mujibu wa (S.w.mwikitionary.org) maana ya ziada ya ndege aliyoikusudia mtunzi ni mwanamke aliyewahi kumpenda kwa uzuri wake na kuridhika kwa sifa zake. Kutokana na kummiliki kwa kila hali ndipo akamnasibisha na NDEGE. Kama anvyosema katika ubeti wa kwanza;

Ndege mzuri ajabu Alitua kitaluni,
Mwenye rangi ya dhahabu Na sauti ya kughani,
Kumtega tajaribu Nimchukue nyumbani.

Kwa upande wa ishara iliyotokana na neon Mtego kwa mujibu wa msimbo wa kiseme limetumika kutoa maana mbili tofauti. Kama inavyoeleweka mtego ni zana maalum inayoweza kutumika kunasia au kukamatia wanyama au wadudu waharibifu (tafsiri yangu) Kwa mujibu wa en.m.wikitionary.org, inaeleza kuwa Mtego "device designed to catch or kill animals" Kwa maana hii tunaweza kusema ni kifaa kilichosarifiwa maalum kwa ajili ya kukamatia au kuua wadudu au wanyama (tafsiri yangu) kwa maana ya pili neno mtego mtunzi amekusudia kama ni mbinu alizozichukua katika kuhakikisha anakipata anachokitaka kama anavyotueleza katika ubeti wa pili. Vile vile msanii ametumia lugha yenye ishara iliyojikita katika msimbo wa kimatukio ambayo imezitawala beti zote katika nyimbo hii ambapo mtunzi anaanza kwa kutuelezea jinsi alivyomuona na kuvutiwa na ndege huyo na kuendelea katika ubeti wa pili kwa kueleza namna alivyotafuta mitego kadhaa na kuhakikisha anamtia mikononi kama anavyo tueleza katika ubeti huu;

Mitego nikatumia Nikaiweka makini,
Na mara akaingia Akanasa mtegoni,
Mwenyewe akaridhia Nikamtia tunduni.

Katika kueleza jinsi gani ndege aliruka anatumia msimbo wa kiishara kwa kutumia neno HASIDI kuwa ni mtu aliyemtorosha hii inatokana na kuwa hasidi siku zote ni mtu wa kuhusudukwa ubaya hivyo, amelitumia neno hili ili kuonyesha na kuashiria kuwa mtu mwenye tabia hii mbaya ya kuvunja mapenzi ya watu ndie aliyemtorosha, hata hivyo anaeleza kuwa juu ya kumchukua kwake kutokana na kukosa kwake huduma na mapenzi ndege hakuweza kuishi na hasidi huyo na kuamua kurudi alikotoka uthibitisho wa hili tunaukuta katika ubeti wa tatu na wa nne anaposema;

Mimi sikutaradidi Kumfatia mwituni,
Mwenyewe leo karudi Yumo mwangu mikononi,
Amenipa na ahadi Ataishi kwa Amani.

#### 4.2.11 Wimbo wa 11: KOMAMANGA

*Komamanga tunda zuri Mtini limetulia,*
*Umbo lake la fakhari Hadhi yake kubwa pia,*
*Kulikosa si khiari Moyo hautoridhia.*

*Tangu utotoni mwake Mate nnalimezea,*
*Sitoki mtini pake Kwenda kuliangalia,*
*Nikingoja siku zote Tunda lipate kupea.*

*Pole pole linakua Nami nalishuhudia,*
*Juhudi nikachukua Mti kuupalilia,*
*Sasa tayari kuliwa Siwezi kuliachia.*

*Wajumbe wako njiani Kwenda kuninunulia,*
*Mwenyewe hatonikhini Najua taniuzia,*
*Apendapo Rahmani Mikononi talitia.*

*KIITIKIO*
*Niradhi nifilisike Lakini nilinunuwe,*
*Sikubali linitoke Lazima nilichukuwe.*

Katika utunzi wa shairi hili la wimbo wa komamanga mtunzi huyu ametumia ishara yenye msimbo wa kimatukio, kiishara, msimbo wa kiseme na msimbo wa kihemenitiki hali iliyopelekea kujenga taswira zenye picha mbalimbali. Kwa kuanza

namsimbo wa kimatukio tunaweza kiliona shairi la nyimbo hii linaelezea tukio la kuchipuka kwa komamanga na kuonekana mtini kitu ambacho kimempelekea mtunzi kuanza kwa kueleza sifa za komamanga hilo tangu udogo wake na ukuwaji wake na kuelekeza jinsi gani alivyokuwa akilishughulikia na kulifuatilia hadi kupevuka kwakekama anvyotueleza msanii katika ubeti wa pili anposema;

Tangu udogoni mwake Mate nnalimezea
Sitoki mtini pake Kwenda kuliangalia
Nikingoja siku zote Tunda lipate kupea

Mohammed Ahmed katika ubeti wa pili anasimulia kukua kwa komamanga hilo na jinsi alivyokuwa analishuhudia na huku akichukuwa juhudi kuupalilia mti ili upate kupea vizuri.Kutokana na juhudi aliyoichukua mtunzi anaamua kulisubiria kulila nae apate ili lisije likawahiwa.Katika ubeti wa nne mtunzi anaonyesha njia sahihi aliyoifuata ili alipate liwe lake ni kutuma wajumbe kwa kwenda kulininua ili alitie mkononi.Kutokana na njia ya usimuliaji wa matukio mtunzi huyu ameashiria kuwa komamanga hili ni msichsana na jinsi alivyomjua na kumuengaenga tangu utotoni kwake mpaka kufikia hatua ya kukua.Mbali na hayo utumukaji wa msimbo huu wa kimatukio unatoa dhamira ya kuonesha njia nzuri ya kujenga mahusiano na hatua sahihi za kuchukua ili mtu kujenga mahusiano yenye maadili kama anavyotueleza katika ubeti wan ne anaposema;

Wajumbe wako njiani Kwenda kuninunulia
Mwenyewe hatonikhini Najua taniuzia
Apendapo rahmani Mikononi tamtia

Katika msimbo wa kiishara msanii ametumia msamiati wa neno Komamanga kuashiria msichana, na mtini kama ni nyumbani kwao.Katika kulisifu komamanga

anaonekana kutoa sifa za msichana aliyevutika nae.Ishara nyengine ni ishara ya utumiaji wa maneno Mti kuupalilia,maneno haya yanaashiria matunzo na huduma alizozitoa kama ni msaada wake kwa kuhakikisha hakuna athari yoyote inayoweza kuathiri ukuaji wa msichana huyo.

Kwa upande wa msimbo wa kiseme umejitokeza katika uteuzi wa neno komamanga ambalo kwa maana ya kawaida ni tunda lenye kokwa nyeupe ndani yake ambapo kokwa zake ndo kinacholiwa katika tunda hilo na kupea kwake ni tunda kupiga rangi njano na nyekundu hata kokwa zake hupiga rangi nyekundu kidogo.Maana aliyoikusudia mtunzi ni maana ya ziada ambapo kalitumia kuashiria msichana aliyemvutia tangu utotoni hadi kufikia kukua kwake kwa kubadilika umbo na kuvutia kwa rangi yake mvuto ambao umempelekea kutuma wajumbe wa kumposa kama alivyosimulia katika ubeti wa nne.Kwa kuangalia msimbo wa kuhementiki ambayo inazingatia utumikaji wa jina la ishara au igizo,mtunzi ameliteuwa jina la nyimbo hii kama ni KOMAMANGA,amekusudia kutoa dhima ya uzuri unaostahiki kuenziwa na kutunzwa kwa gharama zote na si busara kukuta kitu kizuri kama lilivyo komamanga ukaliharibu ujuwe kwamba unajenga mche mbaya kwa jamii.

### 4.2.12 Wimbo wa 12: NDEGE WANGU

*Ndege wangu kaumbika* *Mzuri asokifani*
*Utadhani malaika* *Anapendeza moyoni*
*Katulia hana shaka* *Yumo mwangu mikononi*

*Ndege huyu kasafika* *Hana ila asilani*
*Mzuri kakamilika* *Mfano wake sioni*
*Umbo lake mepambika* *Kimo chake wastani*

*Ajabu uzuri wake* *Hapanapo duniani*
*Mweupe manyoya* *Yake yanapendeza laini*
*Taratibu mwendo wake* *Huringa ringa hewani*

*Ndege huyu kero hana* *Anatulia tunduni*
*Yeye hajui kununa* *Na hafanyi kisirani*
*Kila unapomuona* *Bashasha zipo usoni*

Msanii ametumia msimbo wa kiishara, kiseme na kimatukio, katika kudhihirisha haya tunaona jinsi alivyotumia neno ndege kama ni ishara inayoashiria mwanamke au mke ambae ametumia ubeti wa kwanza kuanza na sifa za ndege huyo. Neno malaika limeashiria sifa nzuri kuumbika kwa mwanamke huyu kama anavyoeleza katika ubeti wa kwanza anasema

Ndege wangu kaumbika Mzuri aso kifani
Uadhani malaika Anapendeza machoni
Katulia hana shaka Yumo mwangu mikononi

Uteuzi wa maneno mweupe, manyoya yametumika kuashiria wasifu wa ndege huyu ambapo katika utunzi wa beti hii ya pili na ya tatu tunapata kuichora picha ya ndege huyu. Katika kukamilisha wasifu ametumia neno tunduni kuashiria nyumbani ndiko anakopatikana ndege huyu. Dhima tunayoipata katika utumiaji wa ishara hizi ni kuleta uhalisia wa sifa za wasichana wachache tu ambao wanaweza kupatikana wakiwa wametunzwa wakatunzika.

Kwa upande wa msimbo wa kimatukio mtunzi anasimulia matukio kwa mpangilio wa beti. Katika ubeti wa kwanza anasimulia muonekano wa ndege mwenyewe kupitia simulizi yake tunapata sifa alizonazo, mbali ya hayo ubeti wa pili na wa tatu unasimulia wasifu wa ndani wa ndege huyo wakati wa tatu anasimulia wasifu wa nje wa ndege huyo. Kutokana na msimbo huu wa matukio tunapata dhima ya kuchunguza wake kabla ya kuwaowa na tabia ni kilema, hivyo mwanamke mwenye tabia mbaya hafai kuwekwa ndani daima habadiliki mfano ubeti wa tatu

Ajabu uzuri wake Hapanapo duniani
Mweupe manyoya yake Yanapendeza laini
Taratibu mwendo wake Huringa ringa hewani

Katika ubeti wa nne anaelezea wasifu wa ndani wa ndege ambae unawakilisha sifa za ndani za msichana aliyempenda.

### 4.2.13 Wimbo wa 13: KUKUPENDA SANA

*Kukupenda sana Ndio kosa langu*
*Sitofanya tena Naapa kwa Mungu*
*Niliyoyaona Yanatosha kwangu*

*Umeisahau Ihsani yangu*
*Umenidharau Kama si mwenzangu*
*Basi angalau Humuhofu Mungu*
*Nikikumbuka Naona uchungu*
*Nilikupokea Kwa hiari yangu*
*Kumenichongea Kukupenda kwangu*

*Nakupenda sana Kama roho yangu*
*Nawe ulinena Wangu pekeyangu*
*Kumbe ni khiana Kwenda kwa mwenzangu*

Msanii katika nyimbo hii ya kukupenda sana amejikita katika ishara yenye msimbo wa kimatukio kuanzia mwanzo wa nyimbo mpaka mwisho wake.Katika hali hii mtunzi amesimulia matukio aliyofanyiwa na mpenzi wakeambae alimpenda kupita kiasi. Mohammed Ahmed anaanza kwa kusimulia sababu ya yote aliyofanyiwa ni kutokana na mapenzi aliyomuonyesha mpenzi wake kama anvyoeleza katika ubeti wa kwanza;

Kukupenda sana Ndio kosa langu
Sitofanya tena Naapa kwa Mungu
Niliyoyaona Yanatosha kwangu

Katika ubeti wa pili anasimulia matukio kadhaa aliyofanyiwa na mpenzi wake yaliyompelekea kujuta kama anavyosimulia katikaubeti huo kwa kusema;

Umesahau Ihsani yangu
Umenidharau kama si mwenzangu
Basi angalau Humuhofu Mungu

Ishara ya pili ya usaliti anaichora katika ubeti wa tatu na wannemtunzi alivyosimulia jinsi alivyompokea kwa mikono miwili na kumridhia kwa kumuamini kwa kumpa mpenzi ya dhati kama anvyosimulia katika ubeti wan ne anaposema;

Nakupenda sana Kama roho yangu
Nawe ulinena Wangu peke yangu
Kumbe ni khiana Kwenda kwa mwenzangu

Dhamira kuu ya utunzi wake kutokana na utumiaji wa msimbo wa kimatukio ni kuonyesha udhalilishaji wa kimapenzi unaopelekea usaliti katika mapenzi.

### 4.2.14 Wimbo wa 14: KWELI ALIKUWA WANGU

*Kweli alikuwa wangu Lakini sasa sinaye*
*Haliwezi pendo langu Nimesha achana naye*
*Bora niwe peke yangu Yamenishinda mamboye*

*Nilimpenda kwa dhati Ikanawiri haliye*
*Aliipata bahati Kila Lake Niridhiye*
*Kumbe vile afiriti Kunidanganya kaziye*

*Nilizikana nasaha Kwa wale wamjuaye*
*Nikampa kila raha Ili kwangu atuliye*
*Malipo yake fedheha Ndio mimi anipaye*

*Sitojifanya tumbili Nikachekwa baadaye*
*Kusamehe afadhali Naale huyo ajaye*
*Atakuta sumu kali Imuuwe hatimaye*

*KIITIKIO*
*Kiasi nimkataye Nalinda yangu heshima*
*Naende amtakaye kwangu mimi nimekoma*

Mohammed Ahmed katika nyimbo hii ametumia nyimbo ishara yenye msimbo wa kimatukio na msimbo wa kiishara, kutokana na usimulizi wa maswahibu

yaliyomkuta ametumia msimbo wa kimatukio kwa kueleza tukio la kuachana na aliyekua mwandani wake kama anavyosimulia kwa kukiri katika ubeti wa kwanza anaposema;

Kweli alikua wangu    Lakini sasa sinae
Haliwezi pendo langu    Nimeshaachana nae
Bora niwe peke yangu    Yamenishinda mamboye

Matumizi ya ishara ya msimbo huu wa kimatukio unasimulia awali ya mapenzi yao jinsi yalivyokua kwa kutumia ubeti wa pili unaeleza jinsi alivyompa mapenzi ya raha kwa kumjali kwa kila hali katika kusimulia hali hii Mtunzi anatumia misamiati kama bahati, ikanawiri kudhihirisha ukweli wa mahaba hayo kama anavyosema;

Nilimpenda kwa dhati    Ikanawiri haliye
Akaipata bahati    Kila Lake Niridhiye
Kumbe vile afiriti    Kunidanganya kaziye

Mbali na hayo, kupitia msimbo huu mtunzi anasimulia jinzi alivyozikana tabia alizoelezwa juu ya mpenzi wake kwa kuona hazina ukweli bali ni fitina tu.Kama anavyosimulia katika ubeti wa tatu;

Nilizikana nasaha    Kwa wale wamjuaye
Nikampa kila raha    Ili kwangu atuliye
Malipo yake fedheha    Ndiyo mimi anipaye

Msanii huyu baada ya kuridhika na aliyoelezwa anatumia ishara hii ya kusimulia tukio kwa kutoa suluhisho lake ambalo analitoa kupitia kiitikio kwa kusema;

Kiasi nimkataye    Natunza yangu heshima
Na ende amtakaye    Kwangu mimi nimekoma

Kwa upande wa msimbo wa kiishara mtunzi ameteuwa misamiati kadha kuwasilisha kwa jamii husika kwa mfano alipotumia neno hafiriti katika ubeti wa pili. Neno hili

linaashiria kutosharifika na kutoridhika na maisha au na hali na katika ubeti huu msanii amelitumia neno hili kuonyesha kuwa mpenzi huyu hakuwa akiridhika naye na wala yale mapenzi ya dhati aliyopatiwa hayakumkidhi hali yake juu ya bahati aliyoipata kwake alionekana kutoridhika na ndio maana alimdanganya.

Uteuzi wa maneno raha, fedheha katika ubeti wa tatu yaanashiria usaliti mkubwa aliyoupata juu ya juhudi kubwa aliyoifanya kama inavyojitokeza;

Nilizikana nasaha Kwa wale wamjuaye
Nikampa kila raha Ili kwangu atuliye
Malipo yake fedheha Ndio mimi anipaye

Mohammed Ahmed ametumia maneno kama tumbili ili kuashiria mtu asiyetulia na uhusiano wa mtu mmoja.Hua anavamia kila anaemuona anamvutia na uteuzi wa maneno sumu kali na imuuwe ni ishara ya tahadhari kwa yoyote atakaye jenga uhusiano naye ajiandae na maradhi ya kuja kumuua.Dhamira kuu ya kutumia lugha ya ishara ya msimbo wa kiishara na kimatukio katika nyimbo hiii ni kuitanabahisha jamii juu ya kuwa waangalifu wanapokuwa na mahusiano ili wasije wakaathiriwa kwa kuambukizwa maradhi yasiyotiba ambayo ni sawa na sumu kali yenye kuuwa.

### 4.2.15 Wimbo wa 15: MPENZI WANGU HAWEZI

*Kala shairi nalia Napukutika machozi*
*Siwezi kujizuwiya Ya michirizi chirizi*
*Nanyi mwaniangalia Wala hamninyamazi*

*Mwenzenu nauguliwa Siupati usingizi*
*Ijapo kula haluwa Wali kwa nyama ya mbuzi*
*Kikumbuka nauguwa Tumbo langu la pumzi*

*Laukuwa namuona Zingelinisha simanzi*
*Hebu jongea Hazina Nikutume yangu kazi*
*Nenda kamwambie mwana Nimekonda kama uzi*

*Madawa nimeletewa* *Sikila hizi na hizi*
*Nyengine za kupikiwa* *Na nyengine za mizizi*
*Lakini kuzichukuwa* *Kuzipeleka siwezi*

*Kama maradhi mzigo* *Wa mpunga au nazi*
*Lau lingekuwa gogo* *Nigeuke mpagazi*
*Au ganda la muhogo* *Nakungojea azizi*

*Maradhi yake nipoe* *Kipenzi changu hirizi*
*Duwa yangu naipae* *Isitimu hata mwezi*
*Naaswe na mumewe* *Likome jambo la wizi*

Katika nyimbo hii ya mpenzi wangu hawezi mtunzi ametumia ishara yenye msimbo wa kimatukio,msimbo wa kiutamaduni na msimbo wa kiishara.Utumiaji wake wa msimbo wa kimatukio unapatikana kupitia usimuliaji wa jinsi alivyoathiriwa na mapenzi ambayo yanamtia simanzina majonzi hata kufikia hatua ya kutoa machozi,kama anavyoeleza katika ubeti wa kwanza anaposema;

Kalashairi nalia Napukutika machozi
Siwezi kujizuwiya Ya michirizi chirizi
Nanyi mwaniangalia Wala hamninyamazi

Katika ubeti wa pili anasimulia jinsi maumivu anyoyapata kutokana na kukosa mapenzi ya uhakika na yenye kuaminika. Maumivu hayo ameyajengea picha kama maumivu ya tumbo la pumzi. Huzuni hizi zinaonyesha kuwa zinasababishwa na kule kuwa mbali na mpenzi wakekwa kipindi kikubwa. Hali hii inajidhihirishia wazi katika ubeti wa tatu anaposema;

Laukuwa namuona Zingelinisha simanzi
Hebu jongea hazina Nikutume yangu kazi
Nenda kamwambie mwana Nimekonda kama uzi

Katika ubeti huu mtunzi aneleza tukio la kutuma kutuma wajumbe ili aonewe Imani na jinsi ambavyo anatuchorea picha ya hali yake alivyodhofika.Kwa upande wa

msimbo wa kiutamaduni Mohammed Ahmed ameonyesha jinsi gani alivyobobea katika lugha kwa kuteua misamiati maalum inayowasilisha utamaduni wa Mzanzibari kwa kutumia maneno kama mizizi,katika ubeti wan ne nawa tano ametumia vyakula maarufu vya kiutamaduni ambavyo ni mpunga na ,muhogo .Kutumia kwake ishara hii ya kiutamaduni kumepelekea kujua jinsi gani ugumu ulioje katika kuhangaikia kile unachokipenda nakutamani kiwe chako ambapo inakubidi uwe na mbinu nyingi ili kuweza kufanikiwa.

Mbali na hayo msanii ametumia msimbo wa kiishara katika kuonyesha shauku na ugumu aliokumbana nao katika kudhibiti na kumiliki inavyostahiki.Katika hali hii mtunzi ametumia neno tumbo la pumzi kuonyesha uchungu na maumivu anayoyapata kutokana na upweke alionao, hali inayompelekea kukosa hata pumzi za kujieleza kwa jinsi ya alivyobanwa.Ishara nyengine iliyojenga picha ya udhaifu wa hali aliyonayo imetokana na matumizi ya tashbiha yaliyoshabihisha binaadamu na kitu .Kama anavyotueleza Khatib(katika mulika 18 anapofafanua kuwa;Tashbiha ni usemi unaolinganisha vitu viwili halisi vinavyoonekana ambavyo vinaleta mshabaha, katika tashbiha maneno kama,mithili au kwamba hutumika (uk77). Hivyo Mohammed Ahmed anatumia tamathali hii kwa kuashiria jinsi hali yake ilivyodhoofu kama anavyoionyesha katika ubeti wa tatu;

> Lau kuwa namuona Zingelinisha simanzi
> Hebu jongea hazina Nikutume yangu kazi
> Nenda kamwambie mwana Nimekonda kama uzi.

Kitika kutoa ishara inayoonyesha ugumu na mbinu mbali mbali alizozitumia kutaka kumrejesha anaeamini kuwa ni mpenzi wake, mtunzi huyu ametumia maneno

kamampagazi, hirizi na dawa ambapo licha juhudi hizo inaonekana kuwa udhibiti wa mpenzi huyo haukuwa kweli kwake ila mpenzi huyo alikuwa amedhibitiwa na mtu mwengine .mwisho mtunzi anaonekana kugonga mwamba kwa juhudi zake na kuamua kuomba dua kamaishara ya kumuachia maamuzi hayo Mumba kama anavyotuthibitishia kwa kusema

| | |
|---|---|
| Maradhi yake nipoe | Kipenzi chake hirizi |
| Dawa yangu na ipae | Isitimu hata mwezi |
| Naaswe na mumewe | likome jambo la wizi |

Dhima kuu ya kutumia ishara hizi ni kuonyesha ugumu uliopo katika kupenda kilichopendwa na kutokana na hali hii anathibitisha wazi kuwa kusicho riziki hakiliki kwani juhudi mbalimbali alizozichukua ili kufanikisha azma yake ya kummiliki mpenzi aliyempenda zimegonga mwamba kutokana na kuwahiwa na mtu mwengine. Vile vile anaiasa jamii juu ya kuwa na maamuzi yenye ukweli katika mahusiano ili kujenga uaminifu katika ndoa

### 4.2.16 Wimbo wa 16: KUDAGANYWA NIMECHOKA

| | |
|---|---|
| *Iwapi ile ahadi* | *Wewe uliyoiweka* |
| *Umenitupa baidi* | *Huwezi kunikumbuka* |
| *Au wafanya kusudi* | *Nipate kuathirika* |
| | |
| *Sikikubwa asilani* | *Kitu nnachokitaka* |
| *Pendo lako la moyoni* | *Wapi unalipeleka* |
| *Hunipi mimi kwa nini* | *Moyoni nikaliweka* |
| | |
| *Itowe yako kauli* | *Mpenzi wangu tamka* |
| *Nijuwe lipi la kweli* | *Kudanganywa nimechoka* |
| *Kataa au kubali* | *Nijuwe hilo hakika* |
| | |
| *Mpenzi wangu tambuwa* | *Vipi ninavyoteseka* |
| *Huwezi kunisumbuwa* | *Na huku ukinicheka* |
| *Si vyema kunizuzuwa* | *Nipe kama unataka* |
| *KIITIKIO* | |

*Kudanganywa nimechoka Mwezio nnateseka*
*Pendo lako nalitaka Nipate kufurahika*

Katika nyimbo hii mtunzi ametumia msimbo wa kimatukio na msimbo wa kihemenitiki ili kuifanya lugha isadifu dhamira zilizokusudiwa kwa jamii katika kusimulia malalamiko yak e juu ya mpenzi wake ambae anaonekana mwenye mwelekeo wa kutaka kumsaliti na ndio maana ananza ubeti wa kwanza kwa kuuliza swali kama anavyosema;

Iwapi ile ahadi Wewe uliyoiweka
Umeitupa baidi Huwezi kunikumbuka
Au wafanya kusudi Nipate kuathirika

Mohammed Ahmed anaendelea kusimulia mkasa wa malamiko hayo ambapo juu ya yote anona kuwa sikikubwa anachokihitaji bali anaonekana kunyimwa kupendwa na aliye mpenda, kitu ambacho si haki kutendewa kwani anaona kwamba aliepewa hakustahiki kama anavyosema katika ubeti wa pili;

Sikikubwa asilani Kitu nnachokitaka
Pendo lako la moyoni Wapi unalipeleka
Hunipi mimi kwa nini Moyoni nikaliweka

Katika masimulizi yake anaonekana kuhimiza kwa kuchora picha ya kusisitiza inayopatikana katika ubeti wa tatu anaposema;

Itowe yako kauli Mpenzi wangu tamka
Nijuwe lipi la kweli Kudanganywa nimechoka
Kataa au kubali Nijuwe hilo hakika

Hata hivyo, mtunzi anaonyesha katika kusisitiza kwa nguvu sasa anamalizia kwa kubembeleza katika hali hii lugha ya ishara inayopatikana kupitia uteuzi wa maneno kama vipi nnavyoteseka. Kutokana na usimuliaji wa malalamiko ya mapenzi ya

udanganyifu, mtunzi anatoa dhamira kupitia matamshi ya kiishara juu ya mapenzi ya udangayifu jinsi yanavyoleta usaliti katika ndoa au katika mapenzi. Kwa upande wa msimbo wa kihemenitiki umelijenga jina la shairi hili kwa maneno mawili ambayo yanajenga dhamira inayojikita katika mapenzi ya usaliti. Msanii anaonyesha wazi kuwa ukweli ni ngao katika mapenzi ya kweli na udanganyifu ni sumu ya mapenzi.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii imeanza kwa kuzifafanua nyimbo mbali mbali zilizokusanywa na mtafiti ambazo utunzi wake umeibua ishara nyingi juu ya hali ya jamii husika. Katika ufafanuzi huo sura hii imebainisha ishara hizo kupitia nadharia ya simiontiki ambayo imejikita katika kufafanua ishara katika kazi za fasihi kwa kuangalia misimbo ya ishara iliyojikita katika mitazamo mitamo. Mitazamo hiyo ni msimbo wa kimatukio ambapo mtafiti ameufafanua kwa kubainisha ishara ya kimatukio ambazo zinajitokeza katika nyimbo alizozikusanya na kueleza dhima ya msimbo huo katika nyimbo hiyo. Katika ufafanuzi huu kumejitokeza baadhi ya nyimbo kuwa na msimbo wa kimatukio pekee na nyengine kuwa na msimbo wa kiishara, kimatukio, kiseme na kihemenitiki na baadhi ya nyimbo zimejengwa na msimbo wa kiishara kimatukio na kiutamaduni mbali na hayo ziko nyimbo zilizojitokeza na ishara zilizojengwa na misimbo yote mitano. Hali hii inatokana na uzito wa dhamira alizozikusudia mtunzi kuzibainisha katika nyimbo zake. Sura hii imehitimishwa kwa kutoa ufafanuzi wa data za upili ambazo zimejumuisha maelezo na majibu ya hojaji zilizotumika katika kuwahoji wasanii, wapenzi na mashabiki wa muziki wa Taarab asilia ambao nao walizieleza ishara zinazopatikana katika nyimbo hizo na dhima zake kwa jamii.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya tasnifu hii ambayo yanatokana na uchambuzi wa data zilizokusanywa na kufafanuliwa hapo awali.Katika matokeo haya tunaweza kusema kuwa ishara zilizotumika katika utunzi wa nyimbo za taarab za Mohammed Ahmed Mohammed zimejigawa katika aina tano (5), Kutokana na mgawanyo huu kuna nyimbo zinaweza zikaingia katika makundi zaidi ya moja hii ni kutokana na nyimbo alizozitunga kuwa ni nyimgi sana na kupitia nyimbo tulizozipata ambazo tumezifafanua nyimbo kumi na tano .Katika kuifanikisha kazi hii kwa kutumia lugha ya ishara iliyotumika katika nyimbo hizo tumeweza kubainisha dhima ya utumiaji wa ishara hizo kwa jamii na kumalizia kwa mapendekezo na matatizo yaliyojitokeza katika utafiti huu pamoja na kuambatanisha viambatisho ambavyo ni nyimbo zilizotungwa na mtunzi huyu.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Kutokana na utafiti huutunaweza kupata matokeoyanayoonyesha kuwa nyimbo za mtunzi huyu zimegawika kulingana na ishara zilizojitokeza na kulingana na kulingana na ishara hizo tunapata dhima mbali mbali kwa jamii.

### 5.2.1 Aina za Ishara

#### 5.2.1.1 Ishara ya Mahusiono

Katika kundi hili zinaingia nyimbo zote alizozitunga mtunziambazo zinaonyesha ishara juu ya mahusiano. Mahusiano hayo yanajitokeza kwa namna mbili tofauti, yapo yale ya ndani ya ndoa na yale ya nje ya ndoa.

Katika mahusiano ya ndani ya ndoa nyimbo zilizojikita katika ishara zenye kuonyesha hali hiyo ni Komamanga, Ndege wangu, Wapenzi wawili, Kukupenda sana, Nanasi, Pendo langu la dhahabu, Tunapendana, Watu wananiuliza, Wawili wanopendana, kati ya nyimbo hizi kuna zile zilizochambuliwa na kufafanuliwa kupitia wahojiwa wake. Kupitia nyimbo hizi jamii inapata kuelimika juu ya uaminifu katika mapenzi, zinahamasisha juu ya umuhimu wa ndoa katika maisha ya kila siku.

Kwa upande wa mahusiano yasiyokuwa ya ndoa msanii ametoa nyimbo ya Kibiriti na petrol, mpenzi wangu hawezi.Nyimbo hizizinatoa dhima ya ukosefu wa amani katika mapenzi, athari ya usaliti wa ndoa.

#### 5.2.1.2 Ishara ya Ujasiri katika Mapenzi

Katika aina hii mtunzi ametumia majina ya baadhi ya wanyama katika nyimbo zake ili kuonyesha ujasiri walionao wapendanao.Katika kuibainisha hali hii nyimbo kama Kunguru, Ndege karuka karudi.Kupitia nyimbo hizi jamii inapata dhamira ya kujenga ujasiri katika maamuzi ya mahusiano ya kimapenzi na kuwa na mapenzi ya dhati.

#### 5.2.1.3 Ishara ya Mapenzi ya Udanganyifu

Kwa upande wa nyimbo alizozitumia kuonyesha ishara hizoni nyimbo ya Kanikimbia, Nilikuchagua, Kisebusebu, Kweli alikuwa wangu, Sitojifanya dhalili ambazo zinaonyesha mapenzi ya udanganyifu.

Kutokana na nyimbo hizo jamii inapata dhima ya kuelimika kwa kujuwa mapenzi ya kweli yanasifa zipi na mapenzi ya udanganyifu yanaathari gani? Na kuelekea katika njia muafaka.

#### 5.2.1.4 Ishara ya Kukataliwa katika Mapenzi

Myunzi ametumia ishara kadhaa katika nyimbo ili kutokubaliwa katika mapenzi kwa mfano nyimbo kamaLishalo haliji tena, Kudanganywa nimechoka, Kweli alikuwa wangu, Pendo kitu cha khiari na Pendo la khiana.

#### 5.2.1.5 Ishara ya Hisia za Mapenzi

Mohammed Ahmed ametoa nyimbo zilizojengwa kwa ishara ya hisia za mapenzi ya dhati. Katika kulidhihirisha hili nyimbo kama Nampenda kumwmbia siwezi, sikujuwa kama mapenzi matamu na Hatupendani kwa pesa. Kutokana na nyimbo hizi jamii inapata dhima ya kujiamini katika mapenzi, ukweli katika mpenzi.

## 5.3 Hitimisho

Sura hii imekusanya matokeo ya tasnifu hii ambayo yamezigawa ishara alizozitumia Mohammed Ahmed katika makundi matano ambazo zinatoa dhamira tofauti ambazo zinatokana na ufafanuzi wa nyimbo hizo. Kumalizika kwa kazi hii kumeweka wazi ishara na makusudio ya mtunzi kwa kuonyesha uhalisia kwa jamii.

## 5.4 Mapendekezo

Tumaini ya kuwa utafiti utapata hamasa na mwelekeo mzuri kwa wasomaji wa kazi hii na nyenginezo za Kiswahili. Aidha itatoa muongozo mzuri kwa watunzi na wahakiki wa nyimbo za taarab na mashairi ya Kiswahili.

Kwa baraza la Kiswahili kuwa na orodha ya kumbukumbu ya wasanii waliokiendeleza na kukikuza katika Nyanja mbali mbali za lugha. Ili kuweza

kupatikana marejeo ya kazi zao na kuendelezwa kwa tafiti za lugha kwa urahisi zaidi.

Kwa upande wa serikali ipo haja kwao kuchukuwa juhudi za makusudi kuhamasisha wanafunzi wa somo la sanaa ya lugha katika maskuli ili kuendeleza na kukuza matumizi sahihi ya untuzi wa kazi za fasihi za Kiswahili.

## MAREJELEO

Adam A. (2009). "Nyimbo za kizazi kipya kwa lugha ya kiswahili Zanzibar." Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha St.Clements.

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (2008). *Utamaduni wa Mzanzibar*. Zanzibara: Quark Express Printing Services Zanzibar.

Barthes, R. (1968). *Elements of Semiology*. New York: HillandWang.

Chama cha waandishi wa Vitabu kanda ya Zanzibar (2007). *Malenga wa Zanzibar*, Express Printing services Zanzibar.

Chandler, D. (2005). *Semiotics for Beginners*. Aberyswyth University. at http;wwwaber.ac.uk/media/documents/s4/semo 20/05/2017.

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Oxford: Claerndom Press Nairobi

Haji, A. (2011). "Mitindo ya nyimbo za Uganga wa pepo." Tasinifu ya Uzamili ya Chuo kikuu cha Dodoma.

Hamadi, A. na Wenzake (1983). *Fasihi simulizi ya Zanzibar*. Dar es Salaam: TPH.

Hassan, T. (2007). "Nyimbo za Msanja na Athari zake Katika Maisha ya Mke na Mume katika Kijiji cha Jambiani." Tasinifu ya Shahada ya Kwanza ya Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Juma, R. (2008). "Nafasi ya Nyimbo za Unyago katika jamii ya Wazanzibar katika zama za utandawazi." Tasinifu ya Shahada ya Kwanza ya Chuo kikuu cha Tiafa cha Zanzibar.

Jilala, H. (2008). "The Artstic uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in new Generation Songs in Tanzania," University of Dar- es-salaam (M.A. Dissertation Unpublished.)

Kondoro, S. (1978). *Ushahidi wa mashairi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: HTL.

Khatibu, M. (1992). *Taarab Zanzibar*. Dar es Salaam: TPH.

Khatibu, M. (2003). "Taarab ni Fasihi simulizi?" Katika makala za semina za kimataifa III, Dar- es- salaam.

Khatibu, M. (2014). Taarab Zanzibar, Oxford University Press Tanzania L.T.D.

Khamis, S. A. M. (2007). "Versality of the Tarab lyrics local Aspects and Gender Influences." in *Kiswahili vol: 70*. Dar- es- salaam: IKR.

Khamis, A. (2013). "Matumizi ya mafumbo na Taswira katika nyimbo za mapenzi za Taarab Asilia ya Zanzibar," Tasinifu ya Uzamili ya Chuo kikuu cha Der-es-salaam.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods&Techniques*. Delhi: New Age International (p) ltd.

Mulokozi, M. (1989). "Uchambuzi wa mashairi," Katika *Mulika 21,* Dar es Salaam: TUKI.

Msokile, M. (1992). "Nafasi ya nyimbo za Fasihi Simulizi katika Jamii." Makala za Fasihi simulizi Chuo kikuu cha Dar- es- salaam.

Mdungi, A. (2007). "Mafunzo ya Nyimbo za Singarimbwa katika Jamii ya Watumbatu." Tasinifu ya Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Mercer, M. (1977). *The Beauty of Zanzibar*. Nairobi: CPI.

Matter, L. (1989). "Tanzu za Fasihi Simulizi." *Mulika na 19*. Dar- es- salaam: TATAKI.

Muhammed, O. (2010). "Mchango wa Nyimbo za Unyago katika Kumkomaza Mwari Kiunyumba." Tasinifu ya Shahada ya Kwanza ya Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Othman, B. na Wenziwe (2015). "Taashira zinazopatikana katika Nyimbo za Mkugo, Tasinifu ya Shahada ya Kwanza ya Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sumait Abdul- Rahman.

Robert, S. (1992). *Wasifu wa siti Bint Saad*. London: Evans Brothers ltd.

Saleh, S. (1990). "Nyimbo za Taarab za Unguja." Katika, *Makala ya lugha yetu Nairobi 37*

Senkoro, F. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: Kauttu L.T.D.

Senkoro F. (1987). *Ushauri – Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: DUP.

Simiyu, W. (2011). *Kitovu cha Fasihi simulizi kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti bookshop. Tanzanian.

Simon, K. (2014). “Ishara katika Kaptula la Marx na Kijiba cha Moyo: Mtazamo wa Kisemiotiki.” Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Thabit, W. (2007). “Nafasi ya Maudhui ya Nyimbo za Taarab katika jamii ya Zanzibar ya leo.” Tasinifu ya Shahada ya Kwanza ya Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasishi: Msingi, na Vipengele Vyake*. Nairobi Phoenix Publishers, L.T.D.

Wamitila, K. (2004). *Kichcheo cha Fasihi*. Nairobi Phoenix publishers.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi za Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers limited.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

www.zanzibits.com/ students/ Ahmad/cu

En.m.wiktionary.org 26/07/2017

Sw.wiktionary.org. 26/07/2017

## VIAMBATISHO

Kiambatanishi A

### SIKUJUWA KWAMBA MAPENZI MATAMU

Ni hakika sikujuwa Kama mapenzi matamu
Sidhihaka nakwambia Yakanitia wazimu
Hivi sasa natambua Kwamba yamenilazimu
Kila ukiniridhia Inazidi yangu hamu

Tafadhali nipe raha Na raha zote zitimu
Unipe kila furaha Zile unozifahamu
Nitononoke kwasiha Kwa yale utonikimu
Wala sifanye mzaha Mwenzio nimadhulumu

Raha zote za dunia Nipe ukitabasamu
Bila ya Kunibaniya Watu wote wafahamu
Yale yanonivutia Yote usiyakasimu
Mwenzio ninaumia Sina akili timamu.

### LISHALO HALIJI TENA

Si kwa ngumi wala fimbo Lishalo haliji tena
Siwezi kula makombo Japo yawe yamenona
Usiyarejeshe mamabo Yalopita mwaka jana

Uganga na Uganguzi Fanya ukifanya tena
Mtishamba na hirizi Ule ukiitafuna
Lakini kwako siwezi Kurudi kudanganyana

Kile nilokitapika Haramu kuramba tena
Ni basi nimetosheka Yatosha niloyaona
Ni bora kukuepuka Si haribu langu jina

Lishalo limeshakwisha
Siwezi kubahatisha
Donda ulonitonesha

La leo siyo la Jana
Wala hamu sina tena
Naapa halitopona

**JUU YA MIBA INOCHOMA**

Juu ya miba inochoma
Vikali imeniuma
Nimetubu nimekoma

Sisubutu kurejea
Nami nikavumilia
Si haba nimeumia

Nimepata maumivu
Kwangu lingaliko kovu
Kumbe roho yako mbovu

Nawe ukachekelea
Bado haijapotea
Kutesa umezoea

Sasa wataka nirudi
Umenitesa kusudi
Kukuepuka sina budi

Uzidi kunioneya
Bila kunihurumiya
Na wala sitorejea

**Kiitikio**

Sithubutu kurejea
Kuteswa sikuzowea

Juu ya miba michongoma
Nimetubu nimekoma.

**KUNGURU**

Kunguru ndege laghai
Kama yeye hatokei
Japo ukifanya rai

Anatabu kumnasa
Mwenye hila na mikasa
Weka mbele kumkosa

Anasifika kwa woga
Ukitaka kumtega
Hutowahi kumpiga

Mwepesi wa kuepuka
Mgumu kuhadaika
Mara moja anaruka

| | |
|---|---|
| Katu humu duniani | Hapana alomueka |
| Kunguru hapatikani | Mjanja wa kusifika |
| Nitumie hila gani | Kunguru nnamtaka |

**Kiitikio**

| | |
|---|---|
| Kunguru ndege laghai | Anatabu kumnasa |
| Japo ukifanya rai | Weka mbele kumkosa |

## NILIKUCHAGUWA

| | |
|---|---|
| Ni bure jeuri yako | Kwako sitoshughulika |
| Usidhani peke yako | Jamali uloumbika |
| Wameenea wenzako | Wazuri wakusifika |

| | |
|---|---|
| Sitishwi na sura yako | Mwishowe itachujuka |
| Ungekua peke yako | Kiasi ungezuzuka |
| Lakini wengine wako | Kwa hilo sitoumbuka |

| | |
|---|---|
| Sitojirahisi kwako | Wala sitobabaika |
| Iwapo sipendwi kwako | Kwengine nitapendeka |
| Duniani wengi wako | Tachagua nnotaka |

**Kiitikio**

| | |
|---|---|
| Nimekuchaguwa wewe | Mimi nawe tupendane |
| Usiponipenda wewe | Watanipenda wengine |

## SASA SINAE

| | |
|---|---|
| Kweli alikuwa wangu | Lakini sasa sinae |
| Haliwezi pendo langu | Nimeshaachana nae |
| Bora niwe peke yangu | Yamenishinda mamboye |
| Nilimpenda kwa dhati | Ikanawiri haliye |
| Akaipata bahati | Kila Lake Niridhie |

Kumbe vile afiriti kunidanganya kazie
Nikazikana nasaha za wale wamjuwae
Nikampa nyingi raha Ili kwangu atulie
Malipo yangu fedheha ndio yeye anipae

Sitojifanya tumbili Nikachekwa baadae
Kusamehe afadhali Ni bora ale ajae
Nae ale sumu kali Imuuwe baadae

**Kiitikio**

Kiasi nimkatae Natunza yangu heshima
Naende amtakae kwangu mimi nimekoma

**KANIKIMBIA**

Hasidi kanikimbia Kaniacha nateseka
Wapi aliokwendea Sipajui kwa hakika
Msiba kaniachia Maisha nitakumbuka

Hasidi huyu katili Kuniua alitaka
Alinitoa akili Nikakonda kwa mashaka
Daima alinidhili Bila ya mimi kutaka

Hasidi alinitesa Na huku akinichekea
Kanimaliza na pesa Sasa nishafilisika
Ndipo akafanya visa Upesi kuniepuka

Hasidi huyu wenzangu Kheri alipoondoka
Kuninyonya damu yangu Hali nikadhoofika
Hiyo ni salama yangu Mauti yangenifika

**Kiitikio**

Sasa ameshanitoka Hasidi wa roho yangu

Shairi:

**MOHAMED AHMED.**

**KISEBUSEBU**

Wajidai hunitaki Wenzio kuwasifia
Kunisengenya huchoki Maovu kunizulia
Kumbe unataharuki Na Mate kunimezea

Kila tunapokutana Uso unanikunjia
Unajidai kununa Nione wanichukia
Wajifanya haja huna Kumbe unaangamia

Wafanya kisebusebu Mapenzi kuyachezea
Pendo ushaliharibu Moyoni lishapotea
Ikikufika aibu Usijekunililia

Waumwa ndani kwa ndani Na huku wavumilia
Nimekwisa kubaini Moyo wako waumia
Wajikaza kisabuni Na huku wateketea

**Kiitikio:**

Wafanya kisebusebu Na kiroho kikopapo
Na kiroho kiko papo

**KUDANGANYWA NIMECHOKA**

Iwapi ile ahadi Wewe uliyoiweka
Umenitupa baidi Hupendi kunikumbuka
Au wafanya kusudi Nipate kuathirika

Sikikubwa asilani Kitu nnachokitaka
Pendo lako la moyoni Wapi unalipeleka
Hunipi mimi kwa nini Moyoni nikaliweka

Itowe yako kauli          Mpenzi wangu tamka
Nijuwe lipi la kweli          Kudanganywa nimechoka
Kataa au kubali          Nijuwe lilo hakika

Mpenzi wangu tambuwa          Vipi nnavyoteseka
Huwezi kunisumbuwa          Na huku unanicheka
Si vyema kunizuzuwa          Nipe kama unataka

KIITIKIO
Kudanganywa nimechoka          Nipe nnachokitaka

## KIBIRITI NA PETROLI

Kibiriti na petroli          Iwapo umeviweka
Hivi ni vitu viwili          Visije kukutanika
Kusalimika muhali          Lazima pataripuka
Bora uvitenge mbali          Hapo utasalimika

Katu haviwi salama          Jambo hili ni hakika
Moto kuja ni lazima          Na wala hapana shaka
Tena tabu kuuzima          Moto ukishakuwaka
Moto wake ni nakama          Lazima kukhasirika

Katu usiviamini          Japo kwa moja dakika
Kabisa havipatani          Mara moja huripuka
Utakuwa khatarini          Huwezi kunusurika
Na jambo hili yakini          Wengi limeshawafika

**KIITIKIO**
Pamoja ukiviweka          hiyo ni khiari yako
Muhali kusalimika          utazuka mripuko

**NANASI**

Nanasi uzuri wake linapendeza machoni
Naipenda ladha yake Nilitiapo kinywani
Ajabu utamu wake Linapumbaza moyoni

Ukiliona nanasi Limetulia dukani
Bei yake ni rahisi Si ghali ni wastani
Kama unayo nafasi Nunua ule nyumbani

Ununuwe liwe lako Lisiwe ni lafulani
Liwe lako mali yako Uwe nalo mikononi
Lako wewe peke yako Ule unapotamani

Usije kulivamiya Chagua lenye thamani
Nanasi lisilopeya Halina ladha kinywani
Utakuja lichukiya Tamu yake huiyoni

**KIITIKIO**

Asiyekula nanasi hajala kitu kitamu

**NAMPENDA KUMWAMBIA SIWEZI**

Kwa mapenzi nnakonda Moyoni nnaumia
Kuna mtu nampeda Daima anisumbua
Jambo moja lanishinda Siri yangu kumwambia

Nimuonapo machoni Sikitiko hunijia
Majonzi tele moyoni Hakika nateketea
Sijui nifanye nini Hata aweze kujua

Namdomo hufungika Maneno hunipotea
Aibu hujanifika Hilo nnalichelea
Ntakuja fedheheka Ataponikatali

Siri nnaibaini Sina budi kuitoa
Naitoa hadharani Ili apate tambua
Sinayo shaka moyoni Mwenyewe atajijua
KIITIKIO
Moyoni nnampenda Na kumwambia siwezi

**MPENZI WANGU HAWEZI**

Kala shairi nalia Napukutika machozi
Siwezi kujizuwiya Ya michirizi chirizi
Na nyi mwaniangalia wala hamninyamazi

Mwenzenu nauguliwa Siupati usingizi
Ijapo kula haluwa Wali kwa nyama ya mbuzi
Kikumbuka nauguwa Tumbo langu la pumzi

Lau kuwa namuona Zingelinisha simanzi
Hebu jongea hazina Nikutume yangu kazi
Nenda kamwambie mwana Nimekonda kama uzi

Madawa nimeletewa Nizile hizi na hizii
Nyengine za kupikiwa Na nyengine za mizizi
Lakini kuzichukuwa Kuzipeleka isiwezi

Kama maradhi mzigo Wa mpunga au nazi
Lau lingekuwa gogo Nigeuke mpagazi
Au ganda la muhogo Nakungojea azizi

Maradhi yake nipowe Kipenzi change hirizi
Duwa yangu naipae Isitmu hata mwezi
Naaswe na mumewe Likome jambo la wizi
**KIITIKIO**
Mpenzi wangu hawezi Kaudhika simuoni

**KOMAMANGA**

Komamanga tunda zuri Mtini lumetulia
Umbo lake la fakhari Hadhi yake kubwa pia
Kulikosa sikhiari Moyo hautoridhia

Tangu udogoni mwake Mate nnalimezea
Sitoki mtini pake Kwenda kuliangalia
Nikingoja siku zote Tunda lipate kupea

Pole pole linakuwa Nami naliangalia
Juhudi nikachukuwa Kwnda kuupalilia
Sasa tayari kuliwa Siwezi kuliwachia

Wajumbe wako njiani Kwenda kuninunulia
Mwanyewe hatonikhini Najua taniuzia
Apendapo Rahmani Mikononi talitia

**KIITIKIO**

Niradhi nifilisike lakini nilinunuwe
Sikubali linitoke Lazima linichukuwe

**NDEGE KARUKA KARUDI**

Ndege mzuri ajabu Alitua kitaluni
Mwenye rangi ya dhahabu Na sauti ya kughani
Kumtega tajaribu Nimchukuwe nyumbani

Mitego nikatumia Nikaiweka mtini
Na mara akingia Akanasa mtegoni
Mwenyewe akaridhia Nikamtia tunduni

Akatokea hasidi Ndege akamtamani
Akafanya ufisadi Kumtorosha tunduni
Na yeye si mkaidi Akamfata porini
Mimi sikutaradidi Kumfatia mwituni
Mwenyewe leo karudi Yumo mwangu mikononi
Amenipa na ahadi Ataishi kwa amani

KIITIKIO
Ndege karuka karudi yumo mwangu mikononi

**NDEGE WANGU**

Ndege wangu kakimbia Mzuri asokifani
Utadhani malaika Anapendeza machoni
Katulia hana shaka Yumo mwangu mikononi

Ndege huyo kasafika Hana ila asilani
Mzuri kakasirika Mfano wake sioni
Umbo lake mepangika Kimo chake wastani

Ajabu uzuri wake Hapanapo duniani
Mweupe manyoya yake Yanapendeza laini
Taratibu mwendo wake Huringa ringa hewani

Ndege huyu kero hana Anatulia tunduni
Yeye hajui kununa Na hafanyi kisirani
Kila unapomuona Bashasha zipo usoni

## MASWALI YA WATAFITIWA

KIAMBATISHO A; Mahojiano na waashiki wa Taarabu asilia Zanzibar

Sehemu A; Taarifa binafsi za mhojiwa

1. Jina kamili la mhojiwa………………………………………………………………………..
2. Mahala mahojiano yanapofanyika……………………………………………………………….
3. Dhamana/cheo au hadhi ya mhojiwa………………………………………………………..
4. Tarehe na muda wa mahojiano……………………………………………………………….

Sehemu B Maswali kuhusu mtunzi wa nyimbo za Taarabu na nyimbo zenyewe.

5. Je unamfahamu mtunzi na mwimbaji wa Taarabu Mohamed Ahmed Moh'd?
   a. ………………………………………………………………………………
   b. ……………………………………………………………………………
6. Kati ya nyimbo zake alizozitunga zipi unazozipenda?
   a ……………………………………………………………………
   B ………………………………………………………………………
   C …………………………………………………………………………
7. Unaionaje lugha ya ishara anayoitumia katika nyimbo zake? Inaashiria nini kwa mfano………………………………………………………………
8. Unafikiria kwa nini mtunzi huyu anapenda sana kutumia lugha ya ishara katika utunzi wake?..........................................................................................................
   ..........................................................................................................................
   .......................................................................................................................
9. Picha gani unazipata katika nyimbo za Mohamed Ahmed?kwa mfano……………………………………………………………………
   ………………………………………………………………………………
   ……………………………………………

10. Ishara alizozitumia Mohamed Ahmed katika nyimbo zake zina dhima gani kwa jamii?........................................................................................../ zinafafanua nini kwa jamii………………………………………………

11. Nini dhima ya utumiaji wa lugha ya ishara katika nyimbo za MOHAMED AHMED kwa msanii, msikilizaji au jamii kwa ujumla………………………………………………………………………… …………………

12. KIAMBATISHO B Dodoso kwa wapenzi na mashabiki wa nyimbo za Taarab za Mohamed Ahmed.

Sehemu A ;

1. Jina la mhojiwa……………………………………………………..
2. Mahali mahojiano yalipofanyika………………………………………………………………..
3. Umri wa mhojiwa…………………………………………………………………
4. Pahala anapoishi na mahojiano yalipofanyika……………………………………………….
5. Muda wa mahojiano…………………………………………………………………
6. Kikundi cha Taarabu anachokipenda……………………………………………………
7. Kati ya nyimbo alizozitunga Mohamed Ahmed ni nyimbo zipi zinazokuvutia
8. Lugha ya ishara anayoitumia katika utunzi wa nyimbo zake inakupa taswira gani unapozisikiliza kwa mfano.............................................................................................................. ............................................................................................................................ ............................................................................................................................ ............................................................................................................................
9. **9.** Katika uteuzi wake wa lugha ya ishara katika nyimbo zake unahisi anakusudia kutoa dhima gani kwa jamii?